

AGANO LA IBRAHIMU

KUTHIBITISHWA



Habari za jioni, marafiki. Vema kurudi tena katika nyumba ya Bwana usiku wa leo, na tayari kuzungumza juu Yake tena, na kushiriki ushirikiano wetu kwa Neno Lake. Ninapenda sana kushirikiana kwa Neno la Mungu, nanyi je?

² Ndio kwanza niambiwe na Ndugu Arganbright, ya kwamba Ndugu Espinoza alikuwa mkutanoni usiku wa leo, alikuwa hapa, na ninafikiri ndugu alisema walitaka aje jukwaani, bali alikuwa amejiepusha na kwenda mahali fulani. Hakika ninakumbuka ule mkutano mkuu huko kwenye Jiji la Meksiko pamoja na Ndugu Espinoza, jinsi Bwana alivyobariki. Huo ulikuwa ndio wakati ambapo yule mtoto mdogo alifufuliwa, ambapo ninii . . . Kamwe sitausahau huo usiku ambao yule msichana ambaye—ambaye alikuwa na yule mtoto mchanga huko kwa ajili . . .

³ Vema, jamani, hapa papa—papa hapa mbele yangu, Ndugu Espinoza, hakika ni furaha kukutana nawe. Mungu akubariki. Ni kama mandhari mazuri ya kuona kwa macho dhaifu. Mungu akubariki. Waweza kuketi chini? Ama u—unaye mke wako ama baadhi yao huko nje? [Ndugu Espinoza anajibu, “Ninaye mke wangu na marafiki kadhaa.”—Mh.] Loo, vema, hilo ni . . . ni zuri jinsi gani. Vema, hilo ni sawa. Nilikuwa nikiwazia tu, mara nyingi nimerejea kwenye hilo, Ndugu Espinoza, jinsi Bwana alivyobariki huko chini Meksiko. Ninaamini nimemwona Dada Espinoza sasa, nina furaha sana kuwaona ninyi nyote.

⁴ Mwajua, wakati sote tutakapofika Mbinguni, itakuwa ni siku ya kushangilia jinsi gani, wakati sisi—sisi sote tutakapoketi chini kwenye chakula cha kutwa cha kimataifa, ama, chakula cha jioni cha kimataifa, ndivyo ilivyo. Nasi tutakuwa, kweli, na wakati mzuri sana tukizungumza juu ya mambo ya kale, na kufanya upya urafiki wa kale, nao utakuwa ni wakati mzuri sana.

⁵ Ninajisikia kama ningeweza kuustahimili mkutano mwingine huko Meksiko; hilo lingekuwa ni sawa tu, tulikuwa na wakati mzuri sana. Ninamkumbuka maskini yule mtoto mdogo, kamwe sitasahau hilo. Maskini mwanamke huyu mrembo wa Kimeksiko alikuwa . . . Billy alinjia, naye akasema, “Baba, itakubidi kufanya jambo fulani.” Akasema, “Hata huwezi kumshikilia mwanamke huyo huko nje.” Kasema, “Wana mabawabu wengi sana,” lakini kasema, “Yeye anataka, kupanda hapo juu kwa vyovyote vile.” Kisha kasema . . .

⁶ Yule ndugu, na—nasahau jina lake ambaye alikuwa pamoja naye, alikuwa akisambaza kadi, ilikuwa ni... Sikuzote nilimwita Mañana kwa sababu sikuzote anachelewa. Alikuwa... Kwa hiyo a—alikuwa aje kunichukua thenashara, ninaamini, naye akanichukua saa tatu. Kwa hiyo nilimwita *Mañana*, “kesho,” mwajua. Naam. Kwa hiyo, naye alikuwa ni ndugu mzuri hata hivyo, ndugu mzuri kweli.

⁷ Nami ninamkumbuka mtoto huyu mchanga. Nikamwambia Ndugu Jack Moore, nikasema, “Vema, shuka uende ukamwombee mtoto huyo nami nitaninii...” Naye Ndugu Espinoza alikuwa akinitafsiria. Basi wakati nikiangalia nje kwenye wasikilizaji upande huu, nao hao watu... nena kuhusu kuja na kuwa waaminifu kwa kanisa, loo, jamani. Walikuja hapo asubuhi; wakasimama kwenye jua kali siku nzima wapate kuwa hapo usiku huo. Mnaona? Na kwa hiyo, wao... Hivyo ndivyo unavyopata kitu. Hapo ndipo unapopata kitu.

⁸ Siyo kwa sababu Ndugu Espinoza yupo hapa, bali nililisema usiku wa kwanza hapa. Hivi majuzi nilikuwa kwenye kanisa fulani, kanisa moja katika mji mwingine, Tucson, Arizona. Na kulikuwako na yapata nusu dazani ya marafiki wangu wa Kimeksiko waliokuwa wametoka mahali fulani, nao walikuwa wameketi hapo siku nzima, siku hiyo, kwenye jengo hilo lenye joto, wakiningojea niwe huko kwa ajili ya usiku huo, walikuwa wameketi hapo siku nzima, wakingojea. Ndipo wakati, nilipoingia jukwaani, nilikuwa nikiomba siku nzima, Nilikuwa nimezungumza asubuhi hiyo kisha nikarudi. Basi usiku huo mara nilipoingia jukwaani, watu hao maskini. Hakika, inawabidi tu kuninii... wanapata... wanazichanganya hizo kadi na kuzisambaza kwa mtu yeyote watakaye.

⁹ Ndipo nilipoitisha mstari wa maombi uliwakosa hao wote, karibu kila mmoja wao. Yapata mwanamke mmoja wa Kimeksiko, nafikiri, alikuwa mle, naye asingeweza kuzungumza Kiingereza, ndipo alipokuja jukwaani, Roho Mtakatifu alishuka, akaanza kuzungumza naye, na kumwambia mahali alikotoka: akamwambia alikuwa na—na mama ama mtu fulani, huko chini kabisa katika huu (Mji huu ni upi chini tu ya mpaka hapa? Ninii... Tijuana.) Tijuana, kule chini, na jinsi alivyokuwa ni mgonjwa, na kasema katika siku kadhaa angepata barua ya kwamba alikuwa mzima na mwenye afya tena. Na mara Yeye alipoanza hilo, ndipo Roho Mtakatifu alipitia moja kwa moja kwa hao wazungu huko nje, akaenda huko ndani, na kumchukua kila mmoja wa hao Wameksiko ambao hata wasingeweza kuzungumza neno moja la Kiingereza, akamponya kila mmoja wao.

¹⁰ Kwa hiyo jambo lilikuwa ndilo hilo. Matarajio! Mnaona? Wewe... Ukifikia mahali ambapo unajinyenyekeza tu, huulizi, ku—kuwa tu mnyenyekevu, ndipo Mungu ataanza kutenda kazi. Atatenda; ni ninii Yake... wakati Yeye kweli atatenda kazi.

¹¹ Sasa, kwa hiyo ninamkumbuka maskini msichana huyu akija, na wakati Ndugu Moore aliposhuka kujaribu kumridhisha, ndipo nikaangalia upande huu, nikaona ono la mtoto mrembo sana wa Kimeksiko, ameketi, akichezacheza, naye hata hakuwa na meno yoyote, akichezacheza tu, akicheka. Nikawazia, “Huyo ni mrembo...Ngoja kidogo,” nikawazia, “huyo ni yule mtoto chini ya blanketi ile.” Kwa hiyo wao... Mdogo...Ilikuwa ikinyesha, naye maskini msichana huyo alikuwa amejifunika blanketi. Naye a—alikuwa amekufa asubuhi hiyo, na hii ni usiku. Nikaenda na kuweka mikono juu ya maskini mtoto huyo, nikamwombea, ndipo akaanza kurusha mateke na kupiga makelele kwa nguvu alivyoweza. Na ni...yeye alifufuliwa na yu hai leo hii nijuavyo mimi.

¹² Sasa, Ndugu na Dada Espinoza mmoja wao, najua walilichunguza hilo kabisa. Na hiyo ni mara tano sasa ambapo nimemwona, kihalisi, akiwafufua wafu wakiisha kufa kwa saa kadha wa kadha (Mnaona?), kuwafufua. Yeye—Yeye ni Mungu.

¹³ Nakwambia, ndugu, dada, jambo ni kwamba, sisi—sisi... Imekuwa...Wakati mmoja kulikuwa...Nitawaambia hadithi ndogo, na ndipo m—mtapata ninalomaanisha.

¹⁴ Kulikuwako na mtu mmoja wakati mmoja aliyesafiri, alikuwa akishuka kwenda baharini. Alikuwa amesoma kuihusu, alikuwa amesikia habari zake, bali kamwe hakuwa amepata kuona ba—bahari kuu. Basi akienda zake alikutana na baharia stadi, ama, baharia, mwajua, akirudi kutoka baharini, ndipo akamwambia, akasema, “Unaenda wapi, rafiki mwema?”

¹⁵ Akasema, “Loo, ninaenda baharini.” Akasema, “Ina misisimko na taharuki.” Akasema, “Sijawahi kuiona,” kisha kasema, “loo, jinsi nimetamani kuiona, kuyaona mawimbi yake makubwa ya chumvi yakiruka hewani, na kuwasikia shakwe wakipiga makelele, kunusa chumvi hewani,” kadhalika namna hiyo, naye akaelezea yote ambayo ingekuwa kwake.

Maskini baharia huyo akasema, “Nilizaliwa juu yake, nimeishi juu yake miaka sitini, sioni chochote cha kuisimua kuihusu.”

¹⁶ Sasa, hivyo ndivyo tu ilivyo. Kuna mambo mengi sana ambayo yametendeka kwenye uamsho huu wa Marekani, hata yamekuwa ni ya kawaida sana kwenu, hata hamtambui kwamba ni nini hasa. Nao watu ambao hawajawahi kuyaona wala kuyasikia, jamani, mioyo ya—yao imejengwa tu na ni tayari na imeenda. Mnaona? Hivyo ndivyo...Yanakuwa ni ya kawaida kwetu. Pia, ndugu, dada, hiyo ndiyo sababu mnanisikia nikiukatakata kwa nguvu niwezavyo, “Uamsho wa Marekani umekwisha.” Ulimalizika yapata miaka minne iliyopita. Kwa hiyo u—umekwisha. Wala hakuna uamsho tena Marekani; tunaokota tu masazo kwenye mashamba ambayo tayari yamevunwa na kuchomwa moto. Unaokota tu ubua mara

moja moja, bali chache sana. Sasa, hatulioni tu hapa Los Angeles ama katika Long Beach; tunalionga kote nchini, vivyo hivyo, kila mahali.

¹⁷ Na mi—mikutano sasa, miamsho mikubwa iko katika nchi za ng'ambo, huko katika—katika nchi zingine, nje ya huku. Na hiyo...ni...Nilikuwa nikizungumza na mmoja wa wamishenari wenu moja kwa moja kutoka kanisani, mvulana anayeketi hapa usiku wa leo, nilikutana na mke wake huko nyuma, ndugu mpendwa, ndio kwanza arudi katoka Gold Coast. Na, loo, jamani, nikasema, “Waonaje?”

¹⁸ Akasema, “Huu—huu kamwe hakutakuwa na mikutano kwangu hapa tena.” Mnaona? Kamwe huna moyo ule ule, unapoenda. Nanyi mnawaona watu wetu wa Marekani wamevalia vizuri sana na kulishwa wala hawana haja na kitu, mwajua, wala hamjui kwamba ninyi ni wanyonge, wenye mashaka, vipofu, maskini, uchi, wala hamjui.

¹⁹ Nawe unawaona wamelala kule mtaani wakifa, mtoto mchanga, maskini tumbo lake dogo limevimba kwa njaa, naye mama anakufa, akijikokota mtaani. Na kuzungumza tu juu ya Yesu Kristo, wana shauku tu na kungojea. Na hebu sema tu jambo moja, nao wako tayari tu. Unapofikia kuondoka ama chochote kile, watakufuata kwenye uwanja wa ndege, “Tuambie tu mara moja zaidi habari za Yesu.” Mnaona? “Heri wenye njaa na kiu ya haki, kwa kuwa watashibishwa.” Hiyo ni kweli.

Sasa, hebu tukiinamishe kichwa chetu kwa muda mfupi tu kwa Mfalme wetu mkuu, kwa—kwa uchaji Kwake, na kuzungumza na Yeye.

²⁰ Baba wa Mbinguni, Wewe ndiwe Mwanzilishi wa Neno hili la Milele. Hapo mwanzo alikuwako Neno; Neno daima alikuwako, kwa sababu alikuwa ni Mungu. Alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu. Na usiku wa leo tunakuona Wewe ungali unalifunua Neno hilo, ukijifunua Mwenyewe kupitia kwenye Neno, na kutuacha tushirikiane kwenye mambo haya makuu.

²¹ Nami ninakushukuru, Bwana, kwa kuwa nia zetu zimeelekezwa huko Meksiko, nchi jirani yetu. Huko chini kabisa miongoni mwa watu hao, ninamkumbuka mpendwa maskini yule mzee kipofu akija jukwaani usiku huo, naye alitaka kutoa rosari yake. Jinsi ambavyo niliuweka mguu wangu karibu na wake, nione kama viatu vyangu vingemwenea, na mabega yangu, nione kama ningeweza kumpa koti langu. Lakini, Mungu, Wewe ulimfanyia jambo kubwa zaidi: uliyafungua macho yake, na jinsi alivyokuwa na shukrani.

²² Ee Mungu, kesho yake usiku nikiliona lile jukwaa limelundikwa makoti machakavu na matambara na kadhalika likajaa hao watu maskini waliokuwa wamejifunika nazo kujikinga na upepo baridi. Loo, jinsi ninavyokushukuru

Wewe, Bwana, ya kwamba, “Heri wenye njaa na kiu, hao watashibishwa.”

²³ Ninaomba, Baba, ya kwamba usiku wa leo, ya kwamba kundi hili dogo hapa litashika ono jipya la Bwana Yesu na Kuja Kwake ambako kumekaribia. Tunaona tuko moja kwa moja katika kule kumalizia sasa kwa Wakati wa Kanisa la Laodikia. Ninawaombea Ndugu na Dada Espinoza, na kazi yao kuu, na upendo wao Kwako, nikijua ya kwamba yeye aliuendeleza mkutano baada ya mimi kuondoka, Nawe ulimbariki; nao viwete wakatembea, vipofu wakaona, viwete, loo, jinsi ulivyowaponya watu katika uamsho mkuu. Nashukuru sana, Bwana, ya kwamba uliwarehemu hao watu wapendwa, wasiojiweza. Mungu, waweza kututuma tena? Tungependa kwenda yakiwa ni mapenzi Yako.

²⁴ Sasa, tunaomba rehema kwa ajili yetu usiku wa leo, na jalia Roho Mtakatifu aje na aingie kwenye Neno tunapojaribu kufundisha tupate kujenga kwa ajili ya ibada ya uponyaji, Jumapili ijayo usiku. Tunaomba, Bwana, ya kwamba viwete watatembea, vipofu wataona, na Roho Mtakatifu mkuu atabariki na kujidhihirisha Mwenyewe kwa njia ya ajabu. Tusaidie kesho, Bwana, pamoja na matangazo na kiamshakinywa cha Wafanyabiashara. Na popote tulipo, jalia tuweze kuitawanya nuru ya mwangaza wa jua kwa wahitaji, na kuwaita wale, Bwana, wanaoona njaa na kiu, wapate kujazwa. Libariki Neno kwenye mioyo yetu usiku wa leo tunaposhirikiana, katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa, usiku wa leo tutajaribu kuendelea katika somo letu katika Kitabu cha Mwanzo.

Kama nikipiga mbinja kidogo, ni—nilivunja pembe moja kutoka kwenye jino moja leo hii, na kwa hiyo kwa namna fulani linasikika ni la kigeni huko juu ninapojaribu kuzungumza.

²⁵ Kwa hiyo sasa, sisi . . . Nilikuwa nikijenga kwa ajili ya ibada ijayo ya uponyaji ya Jumapili hii ijayo jioni. Na sasa, kesho usiku, Bwana akipenda, tutaishia Sodoma, ama Mlimani ambapo Ibrahimu alimpeleka mwanawe kwa ajili ya sadaka; Nafikiri litakuwa ni somo zuri pale la kutuingiza kwenye ibada hiyo ya uponyaji kwa ajili ya Jumapili, kwa kuwa kweli inaelezea pale, jinsi hasa itakavyokuwa kwenye siku hii.

²⁶ Na jana jioni mimi . . . Mara nyingi katika kuzungumza, kukata, simaanishi kuudhi. Ni—ninamaaisha tu kutia neno nanga. Mnaona? Kwa sababu ni—ni wakati ambapo tuna—tuna . . . Nina bidii ya kanisa. Ni—ninayo. Mimi . . . Ninapoliona kanisa likiingia ulimwenguni, linanirarua tu vipande-vipande; kamwe siwezi kusimama kimya. Sasa, simaanishi kuwa tofauti; Mungu anajua hilo; simaanishi kuwa tofauti. Ninawapenda kupita kiasi cha kuweza kufanya hivyo, kuwa tofauti. Lakini wakati ni—ninapoyaona mambo, na kujua kwamba ni kweli, ndipo mimi . . . kuna jambo fulani tu ndani yangu, kamwe siwezi

kutulia; inanibidi tu kulinena, maana . . . Nami ninazungumza tu kwa uvuvio kwa vyovyote vile na kwa hiyo si—simaanishi kuudhi. Lakini na—nawataka mlichukulie hivyo.

²⁷ Na sasa, ili kwamba mpate kuelewa, sisi sote tutakubali ya kwamba tunaishi katika Wakati wa Kanisa la Laodikia; sote tunajua hivyo. Sasa, kumbukeni, kwenye Wakati wa Kanisa la Laodikia, wakati pekee wa wowote wa hizo ambapo Yesu aliwekwa nje ya kanisa Lake Mwenyewe, akibisha mlangoni akijaribu kurudi ndani, na hivyo ndivyo tumefanya, hivyo hasa. Hivyo ndivyo makundi ya Kipentekoste yamefanya kwa sababu daima ni makanisa. Katika kila wakati imekuwa ni kanisa la Kipentekoste. Kama ukisikia matangazo kesho, nitazungumza juu ya hilo. Na kwa hiyo tafuteni kujua kama hiyo si kweli. Ni kweli sikuzote.

²⁸ Tunaposikia juu ya—ya kanisa, kanisa, linapotajwa, katika Biblia, ni kanisa la Kipentekoste. Kamwe halijashindwa kuwa. Kumekuwa na walio wachache wa Kipentekoste kote kote kupitia kwenye kila wakati, na endapo mtaichukua historia.

²⁹ Ndugu Paul Boyd, nimjuaye, rafiki yangu yupo hapa ndani mahali fulani, naam. Nakushukuru, Ndugu Paul, kwa ajili ya kitabu hicho kizuri sana ulichonitumia. Nami nimechukua Nikea, Baraza Lililotangulia lile la Nikea, Baraza la Nikea; na wengi wa hawa wahudumu wananukuliwa vizuri zaidi, ama, wa—wamebobeza vizuri zaidi juu ya hayo, kuliko nilivyo mimi. Lakini ilikuwa ni katika Baraza la Nikea; ilikuwa ni wale masalio wa Pentekoste waliowalazimisha watoke, nao wakaingiza mawazo yao wenyewe ambako kanisa, lile fundisho la Wanikolai, ambalo kwanza lilikuwa ni m—msemu mdogo miongoni mwao. Ilikuwa ni . . .

³⁰ Nalo *niko* ni neno linalomaanisha “kushinda,” *laitia* linamaanisha “kushinda laitia.” Kwa maneno mengine, walitoa roho yote kutoka kwenye kusanyiko, walei, na kufanya mtu mtakatifu kutoka kwake. Acha . . . “Watu si watakatifu kwa hiyo ku—kuhani mtakatifu, askofu mtakatifu, ama kitu fulani . . .” Nalo *niko*, “kushinda laitia” na kuifanya mtu mmoja. Kwa hiyo wote wangeingia, na kulijenga kanisa, na kulipia, na kadhalika namna hiyo. Mtu mmoja tu angeweza kuwa mpatanishi kusamehe dhambi.

³¹ Lakini hiyo siyo tiba ya Mungu. Mungu hatushughulikii kama kanisa; Yeye hutushughulikia kama mtu binafsi. Kwa hiyo Roho Mtakatifu yuko katika walei, kadiri tu alivyo hapa juu ama mahali popote.

Na—nasi tunaona ya kwamba katika hilo, wakati huo walimwondosha Ro—Roho Mtakatifu kanisani, nao wakaliunganisha kanisa na taifa.

³² Wala Konstantino hakuwa mwongovu, mtu aliyefanya mambo hayo. Yeye alikuwa tu kama Ahabu; alikuwa ni

mwanasiasa. Aliichukua tu Rumi ya kipagani na Rumi ya Kikristo na kuyaunganisha pamoja, kisha akachukua ushirikina wa Kikristo, na sherehe za kikafiri na kuzifunganisha pamoja, na kufanya dini ya ulimwengu mzima kutoka kwake kuuimarisha ufalme wake. Yeye hakuwa mwongofu. Yeye... Mambo aliyofanya yalithibitisha ya kwamba hakuwa. Kwa hiyo yeye... Hakika mimi si hakimu wake, bali ninazungumza tu kutoka—kutokana na vile historia inavyosema.

³³ Halafu basi, hapo likapitia kwenye ule Wakati wa Giza, kanisa lilipitia. Hapo unatokea pamoja na Martin Luther, halafu pamoja na John Wesley, halafu kwa Pentekoste tena. Sikuzote limekuwa ni kanisa la Kipentekoste. Nanyi angalieni kote katika nyakati hizo, mnapofananisha na Paulo Mtakatifu wa kanisa la Efeso, kisha mumchukue Ireneo wa wakati wa kanisa uliofuata, Mtakatifu Martin wa hilo lingine, Columba wa hilo lingine, halafu Luther, Wesley, na kuendelea moja kwa moja hata siku hii ya mwisho: sasa tunamtazamia mjumbe mkuu zaidi katika siku za mwisho, ambaye atakuwa ni kuja kwa pili kwa Eliya. Ni kuu.

³⁴ Kama mkiangalia, Yesu alisema kuninii... Kama mnaangalia, tunayo mambo mengi sana kama hayo; inakupasa kuangalia yale unayozungumzia, kwa sababu kila mtu ni Eliya. Tunaye kila mahali sasa na kila kitu kingine, bali huo—huo ni uongo. Huo ni uongo tu uwezavyo kuwa.

³⁵ Na kwa hiyo, mtaona katika Ufunu... katika Malaki yule nabii wa mwisho, katika sehemu ya mwisho ya—ya mlango wa 4, yeye alisema, “Kabla haijaja ile siku iliyo kuu na ya kuogofya ya Bwana, nitawapelekea Eliya nabii.” Sasa, angalieni. “Naye ataigeuza mioyo ya watoto... mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao.”

Sasa, kama mkiangalia, wanafunzi walimwuliza, “Mambo haya yatakuwa lini? Ni kwa nini,” wakasema, “kwamba Eliya hana budi kuja kwanza?”

³⁶ Akasema, “Amekuja tayari,” Yesu alisema, “nao wakamfanyia yale yaliyoandikwa.” Ndipo wakafahamu ya kwamba Yeye alinena juu ya Yohana Mbatizaji. Yeye alikuwa ni Eliya; ni kweli. Lakini ninyi angalieni; kuna kuja maradufu hapo. Huyu asingeweza kuwa ni Eliya halisi aliyepaswa kuwa, kwa sababu Eliya huyu atakapokuja, ilikuwa ni wakati Yeye alipokuwa anaenda kuiteketeza dunia kwa... na wenye haki watembee juu ya majivu ya waovu. Mnaona, ingekuwa—ingepaswa kuwa na—na kwa hiyo huyo hakuwa ni yule Eliya. Yeye ndiye mjumbe wa mlango wa 3 wa Mal-... “Tazama ninamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.” Huyu alikuwa ni Eliya.

³⁷ Basi angalieni hapa, Eliya wa kwanza alikuwa aje, angeigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ama, mioyo ya

baba iwaelekee watoto wao. Mnaona wale wazee wetu wa kale, wale wazee wa kiorthodoksi, washika sheria, torati, aliwageuza kwenye—kwenye imani ya baba zao, hapa, kwa watoto wao, mioyo kwa watoto, Ujumbe huu mpya ambao Yohana alikuwa akihubiri (Mnaona?) wa kule kukaribia kwa kuja kwa Masihi. Yeye aliigeuza mioyo kuelekea kwenye hili.

³⁸ Lakini angalieni wakati—wakati mwingine Yohana anapoonekana, yeye anaigeuza mioyo ya watoto ielekee imani ya baba zao wa Kipentekoste. Kwa hiyo ingekuwa ni kuurudia Ujumbe wa asili. Nasi...mtajua—mtajua wakati utakapofika hapa. Utakuwa wa kurudishwa kulituma kanisa hilo vuguvugu la Laodikia lirudi kwenye ile imani ya asili huko nyuma tena. Naam, bwana. Naye atatiwa mafuta kufanya hivyo. Wakati huyu Eliya ajapo, yeye atakuwa ni nabii. Hatacheza; atakatakata kulia na kushoto.

³⁹ Atachukua ninii yake...atachukua tabia ya Eliya. Mwangalieni Eliya; angalieni kile alichokuwa. Yeye alikuwa nini wakati alipokuja katika wakati wa Yohana? Aliyachukua madhehebu: “Enyi Mafarisayo, msiwazie kusema mioyoni mwenu, ‘Tunaye Ibrahimu Baba yetu,’ kwa maana Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Vivyo hivyo na Eliya. Wote wawili waliwachukua wanawake, ama, wanawake watovu wa uadilifu, na kadhalika waliofanya mabaya. Mwangalie Eliya pamoja na Yezebeli. Mwangalieni Yohana Mbatizaji pamoja na Herodia. Mnaona? Wote wawili ni watu wa nyikani, walipenda misitu, na huko nje. Atoke moja kwa moja vichakani na kuutuma Ujumbe. Atajitokeza jukwaani moja ya siku hizi. Hiyo...

⁴⁰ Naam, na huenda isiwe ni mtu mmoja tu. Lakini itakuwa ni Ujumbe kanisani. Roho Mtakatifu kanisani kuigeuza imani hiyo iirudie ile imani ya asili tena. Hiyo ni kweli, kwa kuwa ataigeuza mioyo ya watoto iwarudie baba zao. Wakati wa kwanza aliigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, wakati huu ni mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, mnaona, akaichukua imani ambayo baba walikuwa nayo, na kuiweka huku kwenye watoto, wale ambao walikuwa wakiingia wakati uo huo. Basi wakati huu yeye ataichukua imani ile ile, maana waliiondokea ile imani ya asili, naye ataigeuza imani ya baba, ama, ya watoto iwaelekee baba zao, wale baba wa Kipentekoste; Matendo 2 nyingine, hiyo ni kweli, nyingine.

⁴¹ Ninalizungumzia hilo asubuhi, Bwana akipenda, *Haikuwa Hivyo Tangu Mwanzo*, kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara Wakristo. Bwana...Hayo ni matangazo, kisha baadaye ninataka kuzungumza juu ya somo la *Kusikia, Kuamini, Na Kulitekeleza Neno La Mungu*. Sasa, na kesho usiku, basi, tutarudi hapa tena kulifunga somo hili la Mwanzo. Kisha Jumapili usiku, Bwana akipenda, tunataka kuwa na ibada ya uponyaji kuwaombea wagonjwa tena, Jumapili usiku.

42 Sasa, sababu ambayo Roho Mtakatifu siku hizi angekemea na kulirarua kanisa, mnakumbuka, wakati wa Laodikia, Yeye anasema, “Wote niwapendao, nawakemea. Wote niwapendao, nawakemea.” Mungu ashukuriwe kwa kukemea; Baba halisi, kutunyosha na kututoa nje.

43 Nilikutana . . . ilitokea nilikutana na mama mmoja leo, naye alikuwa amefadhaishwa sana na yale niliyosema hivi majuzi usiku kuhusu wanawake kuvaa nguo ndogo, fupi: “Haikuwa ni vema kwa Wakristo kufanya hivyo, na ilikiuka maandiko kabisa.”

Akasema, “Kijana, uta—utaiangamiza huduma yako.”

Nikasema, “Loo, la, la. Nisipofanya hivyo, itaangamia. Mnaona?” Akasema . . . Nikasema, “Una hatia?”

Akasea, “La, bwana, mimi sivai kaptura.”

Nikasema, “Vema basi, kwa nini unahangaika?”

Akasema, “Mimi huvaa suruali ndefu.”

Nikasema, “Hizo ni mbaya zaidi.”

44 Akasema, “Loo, la,” akasema, “ni—ni—ni za heshima hivyo.” Kisha kasema, “U—unazivaa, kama, utafanyaje na mwanamke aliye huko kondeni?” Ninaamini ni vile alivyolisema, kasema, naam, “Kumwendesha farasi,” kasema, “huko nje na mume wangu kusaidia kuwakusanya ng’ombe, unafikiri ninapaswa kuvaa sketi? Kwa kuwa wewe ni . . .”

45 Nikasema, “Haikupasi kuwa huko nje kwanza. Hiyo ndiyo shida yake; wanawake wanajaribu kuchukua kazi za wanaume sasa; tunao wanaume wengi sana wasio na kazi.” Kweli, hiyo ni kweli.

46 Kasema, “Vipi kuhusu shambani wakati una—wakati unapong’oa vitu, shamba huku u—umevaa gauni. Hufikirii ingekuwa bora zaidi ni—nikiwa na suruali ndefu?”

47 Nikasema, “La, mama. Mke wangu hana shida nalo, wala mama yangu. Sidhani utakuwa nayo pia, ikiwa tu utajichunga.” Nikasema, “Sidhani, kama—kama . . .”

Akasema, “Kwani suruali ndefu ni mbaya?”

Nikasema, “Biblia ilisema ya kwamba mwanamke atakayevaa vazi lolote limpasalo mwanamume, ni chukizo machoni pa Mungu.” Hiyo ni kweli.

48 Ndugu, Maandiko yote yako hapa; hebu na tuyatii tu. Hivyo tu. “Wote niwapendao, nawakemea.” Hiyo ni . . . wakati huu, hiyo ni kweli? Kwa hiyo, halafu basi, Biblia ilisema, pia, katika Waebrania mlango wa 12 na kifungu cha 8, “Na kama hawawezi kustahimili, wala hawatavumilia kukemewa, wao ni wa haramu wala si wana wa Mungu.”

49 Mwanamume analipuka, “Huump!” Mwanamke, “Loo, sitasikiliza hilo tena, sio lazima mimi...” Vema, endelea, ewe mwana haramu. Hiyo ni hakika.

50 Lakini mwana halisi wa Mungu atakubali kusahihishwa, akisema, “Naam, Baba, ni Neno Lako; Inanipasa kujinyosha sasa; sina budi kufanya yaliyo mema.” Mnajua hiyo ni kweli, sivyo? Mwana haramu ndiye sikuzote anarudi nyuma na ndiye kisirani, kwa hiyo, akijaribu tu kuvuruga kitu fulani. Lakini mtoto halisi wa Mungu hupendelea kukemewa na kunyosha.

51 Kamw-...Mzee babangu kamwe hakunicharaza wakati mmoja pasipo mimi kubariki kila kichapo alichonipiga kunifanya kile...Kama isingalikuwa hivyo, mbona, labda mimi mwenyewe ningekuwa haini. Kwa hiyo mimi...Hiyo ndiyo shida ya kina Riki wengi wadogo kupita kiasi na kadhalika siku hizi. Mnawaachilia wakimbie huku nje, na kujitupatupa kote, kufanya vishindo kwa miguu yao; na maskini Mary, “Sitafanya hivyo.” Yeye ka-... alipaswa awe na mama yangu. Hiyo ni kweli. Um-hum. Naam, bwana.

52 Tunawaachilia watoto kupita kiasi sasa...Si ajabu tuna upotovu wa vijana. Mnajua ni kitu gani kilichousababisha? Upotovu wa wazazi. Hilo ndilo lililouanzisha. Naam, bwana. Hamkuwaweka watoto wenu karibu nanyi. Mkawaachilia kwenda nje katika sehemu hizi na kuendelea namna hiyo, na kuliunga mkono. Si ajabu tuko katika wakati kama huu tuliomo sasa.

53 Sasa, mambo haya hayapendwi na watu. Hiyo ndiyo sababu huduma yangu haijapanuka, ama, si kubwa kama za jamaa hao wengine. Na kama kamwe ikienda hivyo, ninataka, “Mungu ibomoe,” kusudi ifikie mahali ambapo ninaweza kweli kwenda na kusema kweli.

54 Mimi—mimi—mimi si mfuasi wa dhehebu lolote, kwa hiyo ninaweza kulikaripia kwa njia yoyote nitakayo. Mnaona? Mimi si mfuasi wa kundi lolote, kwa hiyo ninaweza kusema nitakayo. Mimi ni wa Kristo tu, nami ninaweza tu kukaa pale pale. Hainibidi kuwa na pesa, kwa hiyo hilo—hilo hapo. Ninadumu moja kwa moja nalo. Ili kwamba popote Mungu anaponituma, ninaenda tu na kulipasua moja kwa moja jinsi Yeye anavyoniambia na kuondoka (Mnaona?), ninarudi tena.

55 Kwa hiyo nasha-...Hivyo ndivyo ninavyolitaka. Sitaki wajibu mkubwa ambapo inanibidi kuombaomba pesa, na kusihi nipate *hiki*, na kuchukua *hiki*, na kuendeleza *hiki*, na jamaa huyu mkubwa. Sina budi kuweka nia yangu juu ya Kristo. Nenda, kajiangelie mwenyewe miongoni mwa ninyi wengine kufanya hivyo. Kwetu sisi, hebu tujitolee kwa Neno la Mungu na—na kuhubiri, kudumu na kweli na ufunuo wa Roho Mtakatifu na yale yatakayotukia.

⁵⁶ Sasa, tunaona... Sasa, hebu tupate msingi kidogo juu ya Ibrahimu sasa. Jana usiku tunaona ya kwamba Ibrahimu alikuwa ni mtu wa kawaida tu. Hiyo ni kweli? Sasa, hiyo ni, leo hii ni, wakati Mungu anapombariki mtu, basi wa—watu wanafikiri hana budi kuwa ni mtu wa kipekee sana, wa kipekee sana. La, ni mtu tu wa kawaida.

⁵⁷ Kumfanya mtu mtakatifu, mtu mkuu, amepitia kwenye vizazi vya watu watakatifu naye hana budi kuwa ndiye. La, hilo silo.

⁵⁸ Biblia ilisema ya kwamba Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi. Alikuwa ni mwanadamu tu. Ibrahimu alikuwa ni mtu wa kawaida tu aliyeshuka chini, mzee aliyeshuka kutoka Babeli, akashuka kwenye nchi ya Wakaldayo na mji wa Uru, mtu wa kawaida tu, yeye pamoja na mkewe, labda mkulima maskini, chochote alichofanya kujipatia riziki.

⁵⁹ Nasi tunaona ya kwamba Mungu alisema naye siku moja na kumwambia ya kwamba atapata mtoto kwa mkewe. Naye alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano na mkewe sitini na mitano wakati huo. Sasa, lilikuwa ni la mapinduzi, kimapinduzi hasa, kuwazia kwamba Mungu angenena hayo kwa mtu mwenye umri wa miaka sabini na mitano. Lakini mnaona, Mungu hufanya anayotaka kufanya, Naye kwa kawaida hufanya mambo kwa njia ya kipekee sana.

⁶⁰ Naye anakufanya utende mambo ya kipekee wakati wowote unapolitii Neno Lake. “Kwa kuwa wote wale ambao wanaishi kitauwa katika Kristo Yesu watapatwa na mateso.” Lakini inakubidi tu kuja moja kwa moja kwenye Neno; usinini—usinini. . . Si la kufasiriwa apendavyo mtu yeyote. Lisome tu jinsi lilivyoandikwa na uliamini jinsi lilivyoandikwa, na jinsi unavyopaswa kuliamini. Na endapo hutalitilia shaka, litatoa kila kitu lilichoahidi. Kama unaweza kuchukua msimamo mzuri wa kiakili ya kwamba Mungu ndiye aliyeliandika Hilo: “Mungu alilisema; ahadi hiyo ni yangu; ninaiamini,” liangalie likitukia. Halina budi, halina budi tu kutukia.

⁶¹ Sasa, tunaona ya kwamba Mungu alimwambia ajitenge mwenyewe (jana usiku) na mbali na jamii yake, mbali na watu wake. Lakini Ibrahimu, kama mtu wa kawaida... Sasa, Mungu kamwe—kamwe hakumfukuza kutoka kwenye... kurudi kwenye nchi ya wenyeji wake kwa kufanya hivyo. Ila Ibrahimu kamwe hakubarikiwa na Mungu mpaka alipojitenga na watu wake wote. Alimchukua baba yake pamoja naye; akawachukua wengine zaidi pamoja naye, akamchukua mpwa wake. Naye mzee huyo sikuzote alikuwa kikwazo, mpaka hatimaye Mungu akamwondosha. Na halafu Lutu, mpwa wake, alirudi nyuma kisha akaenda huko chini Sodoma. Basi—halafu basi wakati alipotenganishwa nao, ndipo Mungu akaanza kumwambia kuhusu baraka, ni... vile atakavyombariki. Napenda hilo.

⁶² Sasa, tunaona katika Mwanzo 13:16, ninii...Mungu alimwambia Ibrahimu, wakati aliponena naye kuhusu agano Lake, Yeye alisema, “Nitakuzidisha, na uzao wako utakuwa kama” mavumbi ya...kwa...“mchanga ulioko pwani,” kama punje za mavumbi nchini. “U—uzao wako utakuwa hivyo; baba wa mataifa.”

⁶³ Na sasa tunaona pia katika Mwanzo 15:5, wakati Yeye alipolithibitisha lile agano, ama aliposema naye tena kulihusu, Yeye alisema, “Basi toka nje, angalia juu; unaweza kuzihesabu nyota?” jinsi ambavyo kuna nyota nyingi sana, zisizohesabika.

⁶⁴ Angalieni, kutoka mavumbini hata kwenye nyota. Loo, jamani, kutoka ardhini, kaburini hata Utukufuni. Nanyi mnakumbuka, ule Uzao halisi ulioahidiwa Ibrahimu, ambao ulikuja kupitia Isaka, ulikuwa ni Kristo. Na “Yeye ni Nyinyoro ya Bondeni, ile Nyota Angavu ya Asubuhi, aliye mzuri kuliko wote wa elfu kumi kwa moyo wangu.” Jinsi tunavyoliangalia hilo, jinsi ambavyo Mungu katika mfumo Wake mkuu wa jua hutangaza. Mnaamini ya kwamba Mungu huishi katika mfumo Wake wa jua? Mnaamini Yeye alizifanya nyota? Alisema alizifanya. Jinsi ambavyo kila kitu kimepangwa kikamilifu sana katika mfumo wa jua. Kutoka kwenye... .

⁶⁵ Angalieni, kutoka mavumbini, hapa chini kuelekea duniani, hata kwenye nyota Utukufuni, Yesu, Nyota Angavu ya Asubuhi, Kichwa cha zote. Yeye kwa kweli ndiye Uzao ulioleta nyota hizi zingine kupitia Kwake. Nasi tunaona ya kwamba sisi tukiwa wafu katika Kristo, sisi ni uzao wa Ibrahimu na ni warithi pamoja na baba Ibrahimu kwa ile ahadi. Basi kama sisi ni uzao wa Ibrahimu, tunaona ya kwamba tunayo—tunayo imani ya Ibrahimu, la siyo sisi si uzao wa Ibrahimu.

⁶⁶ Basi Uzao wa Ibrahimu ni nini? Roho Mtakatifu (Amina!) anayekuja kupitia kwa Kristo Yesu, hilo linatufanya, tunapompokea Roho Mtakatifu, basi sisi sio, sio Wamataifa tena, bali sisi ni Wayahudi. Naye Myahudi, kwa kuzaliwa, si Myahudi. Paulo alisema, “Yeye si Myahudi aliye kwa nje: bali kwa ndani,” aliye na imani ya baba Ibrahimu. Basi kama sisi ni uzao wa baba Ibrahimu, basi tunachukua kila ahadi Mungu aliyoifanya, haijalishi jinsi linavyoonekana la kimzaha, jinsi ha...jinsi ambavyo lisingeweza kutukia; bali kama Mungu alisema hivyo, tunaliamini kwa vyovyote vile.

⁶⁷ Sasa, Ibrahimu, wakati alipopaswa kumpata mtoto huyu, tulipitia hilo jana usiku, wakati huenda Sara alisema baada ya siku za kwanza ishirini na nane, yeye alisema, “Unajisikiaje, mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Mungu asifiwe, tutampata kwa vyovyote vile.” Wala hakuwa dhaifu hata kidogo; alipata nguvu zaidi wakati wote, “Naam, nitampata mtoto huyo kwa vyovyote vile.”

⁶⁸ “Unajua je kwamba utampata? Mbona, wewe ni—wewe ni mzee zaidi, unazeeka zaidi. Vema, una miaka sabini na mitano; umeishi naye tangu alipokuwa na miaka kumi na minane, ama kitu fulani,” dada yake wa kambo. “Na sasa unajua hilo haliwezekani; wakati ulipokuwa mdogo, ulipokuwa kijana, na labda wakati wewe . . . yeye alipokuwa na kumi na minane, nawe ishirini na minane.” Kulikuwako na tofauti ya miaka kumi katika umri wao. “Vema, huo ndio wakati ungalimpata huyo mtoto kama ulikuwa umpate mmoja. Lakini miaka hii yote, na sasa amekoma hedhi kwa miaka na miaka na miaka, basi utampataje mtoto huyo? Haiwezekani.”

Vema, daktari akamwalia, kasema, “Maskini jamaa huyu mzee amerukwa akili, wajua, yeye . . . kuna kasoro.”

⁶⁹ Hivyo ndivyo wanavyosema juu ya kila mzao wa kweli wa Ibrahimu. Wao tu ni, “Loo, usinini, achana tu naye, hatadhuru kitu, hana uwezo, lakini, unajua, wala hana matumaini pia,” wanafikiri. Lakini anamwamini Mungu.

⁷⁰ Jamaa aliyekuwa na ahadi angeweza je, kama vile Musa akishuka kwenda kuitaka Misri, mtu mmoja akiwa na fimbo mkononi mwake? “Akishuka kwenda kuitaka.”

“Unajua je utaiteka?”

“Mungu alisema hivyo, hilo latosha.” Hiyo ni kweli. Uzao wa Ibrahimu tena. Mnaona? Yeye alikuwa—yeye alikuwa na imani ya Mungu kwa sababu alikuwa ni uzao wa Ibrahimu.

⁷¹ Na sasa, tunaona jana usiku ya kwamba yeye alikuwa Abram mpaka Mungu alipombariki na kufanya agano naye, Ndipo basi akabadilisha jina lake kutoka Abram likawa Ibrahimu. Na h-i-m-u ilikuwa ni sehemu ya Jina la Mungu. Mliona hilo? Hivi lilipata kukolea ndani? Ibrahimu. Elohimu. Mnaona? Yeye aliweka sehemu ya Jina la Mungu kwa sababu Mungu ni Baba ya wote. Naye akafanya Jina Lake, akiwa ni Elohimu, Yeye aliweka sehemu ya Jina Lake na Ibrahimu (Mnaona?), na kumfanya mwenziwe. Kupitia uzao wake Yeye angeleta Uzao na kulibariki kila taifa duniani. Angekuwa baba wa mataifa mengi. Ibrahimu angeleta tena imani ya Elohimu, h-e-m-u na h-a-m-u. Lakini Yeye alimfanya sehemu ya Jina Lake kwa sababu alikuwa awe baba wa mataifa mengi.

⁷² Loo, lina utajiri sana, laiti tungalikuwa na wakati wote; tungeuchukua tu na kusoma tu kifungu kwa kifungu na kulipitia. Nawaambia; linanifanya tu karibu kuruka katika Mbingu ya saba, ku—kuwazia jinsi Biblia hiyo ilivyo kamilifu. Hakuna Andiko moja linalopinga lingine, kamilifu tu kabisa kabisa liwezavyo kuwa. Hakuna hitilafu katika Biblia. Jamaa anayesema hivyo, mlete tu huku. Hakuna kitu kama kuhitilafiana katika Biblia ambacho hakiwezi kunyoshwa na Neno la Mungu. Hiyo ni kweli. Sasa, yote imejaa mafumbo, kwa sababu Yeye ameifanya hivyo apate kuificha kutoka kwa

macho ya wenye hekima na wenye elimu na kuwafunulia watoto wachanga wanaoweza kujifunza. Naam.

⁷³ Sasa, ninaye mke; jinsi ninavyompenda; mwanamke mzuri kuliko wote duniani kwangu mimi. Sasa, sisi si... sisi ni... Tunaamini katika... tunaamini ya kwamba Mungu ni upendo. Na kama Mungu ni upendo, basi Yeye anatupenda sana hata akamtoa Mwanawe pekee tupate kuokolewa. Sasa, ninapoenda kwenye nchi za ng'ambo, simwiti Bibi Branham ndani, niseme, "Bibi Branham mpendwa, nina ziara ya nchi za ng'ambo; usiwe na waume wengine wakati nimeondoka. Usimkonyezee macho mtu yeyote wakati nimeondoka."

⁷⁴ Hayo si yangekuwa... na kama angenishika tai na kusema, "Ngoja kidogo, Bw. Branham, usiwe na wake wengine wala hata wapenzi, wakati umeondoka." Sasa, hiyo si ingekuwa ni nyumba? La. Hivyo sivyo. Kama ingekuwa hivyo, ningehofu wakati wote; naye pia.

Lakini jambo ni kwamba, ni—ninampenda. Nami nitasema, "Mpenzi, Bwana ameniita kwenda nchi za ng'ambo."

"Vema, Bwana ashukuriwe." Yeye hana budi kukaa nyumbani, mwajua, na kuwashughulikia watoto.

⁷⁵ Na kwa hiyo, tunafanya nini? Tunapiga magoti sakafuni na kuomba, tunawaleta watoto wetu hapo na kuomba. Naye anaomba, "Mungu, mlinde Bill; si—siwezi kuwa msaada sana ila nita—nita—nitafanya yote niwezayo hapa pamoja na hawa watoto."

Ndipo ninambusu kwaheri, "Kwaheri, mpenzi."

⁷⁶ Mradi tu ninampenda hivyo, usijali; mradi tu ananipenda hivyo, hakuna hofu ulimwenguni. Si kile ninacholazimishwa kufanya; ni kile ninachofanya kwa upendo.

⁷⁷ Na hivyo ndivyo ilivyo na Mungu. Tu—tunaacha kufanya mambo haya, sio kwa sababu, twasema, "Vema, si—si—si—si—sipaswi kwenda kwenye sinema; si—sipaswi kucheza dansi; sipaswi kuvuta sigara; sipaswi kunywa pombe, maana mimi ni Mkristo sipaswi kufanya hivyo, hata hivyo ninataka kulifanya." Hata afadhali ulifanye. Hmm? Ukimpenda Mungu, u—unalifanya tu kwa saba—... hulifanyi kwa sababu unampenda Mungu. Unaona?

⁷⁸ Sasa, vipi kama nchi za ng'ambo, kama ningerudi, nami nilimchukua mwanamke fulani, na kumpeleka mahali fulani tukiendesha, nirudi na kumwingiza ndani, kasema, "Usiku mwema kwako," na kadhalika. Na—na—nami ni—ninajua itanibidi kumwambia Meda kuhusu hilo. Vema, ninaamini angenisamehe hilo.

Ni—ni—ningesema, "Meda, ni—nilifanya hilo." Ningeenda kulikiri na kusema, "Nilifanya hilo. Sa—samahani nililifanya."

⁷⁹ Yeye...Ninajua angesema, “Bill, nitakusamehe hilo.” Lakini hilo lingenifuata siku zangu zote zilizosalia, maskini jamaa huyo, ninajua nini, jinsi ninavyompenda. Haidhuru ilinibidi kupitia nini, nisigemwudhi kwa chochote kile. Ninampenda kupita kiasi. Mimi...Huo ndio upendo wangu kwake. Naam, bwana.

⁸⁰ Ni—ninaondoka nyumbani, kutoka kwa watoto wangu, wakati moyo wangu unatamani sana kuwa kule pamoja nao. Mtoto Joseph aliniita, hivi majuzi, wakati nilipokuwa nikiondoka; anajua wakati mwingine mabadiliko ya maji hutufanya wagonjwa. Akatoka nje; alitaka kuja pamoja nami sana, alikuwa akilia asubuhi nzima. Basi akatoka akaja barazani; akaangalia nje, na kuunyosha mwili wake mdogo, kisha akayapangusa macho yake makubwa, akaangalia nje, akasema, “Baba?”

Nikasema, “Naam, mwanangu?”

Akasema, “Mungu akubariki, na naomba kamwe usiwe mgonjwa,” umri wa miaka minne tu, jamaa mdogo. Loo, jamani.

⁸¹ Jamaa huyo mdogo huona maono na kila kitu. Mimi... Siku moja nitakapomaliza, ninataka kuichukua Biblia yangu na kuikabidhi mkononi mwa Joseph, na kusema, “Kipenzi, dumu pamoja nayo; usipatane juu yake; kaa papo hapo. Ninakutaka udumu pamoja na Neno.”

⁸² Na kwa hiyo, jambo ndilo hilo; ni upendo. Ingawa ninajua kama nikifanya jambo lolote baya, ninaamini Mungu angenisamehe hilo. Lakini, loo, jamani, nisingetaka kumwudhi. Nisingetaka kufanya lolote kumwudhi. Ninampenda kupita kiasi. Vema, hivyo ndivyo tunavyopaswa kumwishia Mungu, kupendana Naye. Upendo, ni kupenda tu hata mpendane mmoja na mwenzake. Yesu alisema, “Hivi watu wote watatambua ya kuwa ninyi ni wanafunzi Wangu mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.” Sio kwa sababu wewe ni Mmethodisti, au Mbaptisti, ama Mlutheri, au Mpentekoste; kwa sababu mnapendana.

⁸³ Na hivyo ndivyo sikuzote nimejaribu kufanya kusudi nizibomoe kuta hizi za kiakili na kupata njia niweze kusema tunapendana. Mnaona? Lakini, mnaona, mradi tu tunafanya mambo tunayofanya... tunaliona pale kama vivuli katika Biblia ambapo walilifanya hapo mwanzo; nanyi mnaona yaliyowapata. “Basi mambo haya yote yalitukia kama mifano,” inasema Waebrania.

⁸⁴ Sasa, tunaona, ni jambo lile lile sasa. Tunajiweka kando, na baridi na kutojali; na kuketi kwenye mlima huu kwa muda wa miaka arobaini badala ya kwenda kwenye nchi ya ahadi.

⁸⁵ Kwa hiyo mavumbi, kutoka mavumbini hadi kwenye nyota. Kutoka kwenye mavumbi ya ardhini, yale tuliyoanyizwa kwake, hata kwenye nyota zing’aa Utukufuni. “Wale wamjuao Mungu wao watafanya kazi kubwa, nao watanawiri kama nyota milele

na milele.” Danieli 12. Naam, watanawiri. Wazieni tu, nyota hiyo ya asubuhi haijapoteza uzuri wake hata kidogo tangu Mungu alipoining’iniza kule kwenye—kwenye mfumo wa jua. Haijapoteza uzuri wake hata kidogo. Itatoweka kwa mabilioni na mabilioni ya miaka, nasi tungali tutakuwa tukinawiri Utukufuni. Naam, bwana. Ni kielelezo tu, mfano tu.

⁸⁶ Ninataka kusema jambo fulani hapa, nami ninahofia kufanya hivyo, nami . . . Ni sawa, ndugu? Loo . . . Sasa, inakubidi kuangalia wakati ukininii . . . hasa sana na watu; wanaelewa vibaya.

⁸⁷ Sasa, ninaamini ya kwamba tatu ni utatu, uko katika mmoja, kama tujavyo. Sasa, ninaamini ya kwamba Mungu alikuwa na Biblia tatu, kama mtaangalia. Sasa, Biblia ya kwanza aliyoandika ilikuwa mbinguni, ile zodiaka. Sasa, ninajua unaweza ukaingia wazimu juu ya hilo, na kuingia wazimu juu ya chochote kile. Lakini kweli, kama mkiangalia zodiaka, ilianza jinsi gani? Inaanza, ya kwanza katika zodiaka ni bikira. Ya mwisho katika zodiaka ni Leo, yule simba, Kuja kwa Kwanza na Kuja kwa Pili kwa Kristo: mara moja kupitia kwa bikira, ya pili kama simba wa kabila la Yuda. Unashika samaki aliyepindika kupitia hilo, wakati wa kaa tunaopitia.

⁸⁸ Kila kitu angani kinamtangaza Mungu; hakika kinamtangaza. Naye Mungu . . . watu walikuwa waangalie juu, wakitambua Mungu wao hayuko duniani, bali Yeye yuko Mbinguni. Yeye aliandika Biblia ya kwanza.

⁸⁹ Sasa, kitu cha pili Yeye alichandika, Henoko, katika wakati wa piramidi, huko chini Misri. Nimekuwa huko na labda wanaume wengi humu ndani, na wanawake, wamekuwa kule. Mnaona piramidi hizo, tusingeweza kuzijenga tena. Ni kubwa kupita kiasi, kubwa kabisa. Ziko kijografia katikati ya dunia sana, haidhuru jua liko wapi, kamwe hakuna kivuli kando ya hizo. Nao wana tani na tani na tani za majabali huko juu ambayo walibishania hilo wakati mmoja. Tulikuwa tukijadiliana hilo shuleni, jinsi walivyozijenga. Vema, jamaa, mpinzani wangu alisema, “Waliyainua kwa kuyabingirisha.”

⁹⁰ “Mbona,” nikasema, “hiyo ni—hiyo ni . . . Mbona, wasingeweza.” Ninajua huwezi kuchukua behewa na kulipakua na kuliweka kwenye reli na kuweka wanaume wa kutosha kulizunguka ili kulisukuma. Haiwezekani, ikiisha kupakuliwa, huwezi kufanya hivyo. Nimeliona likijaribiwa mara nyingi mno. Unaweza tu kuweka mstari mmoja wa watu. Mstari huo mwingine hauna budi kuusukuma mgongo wa mtu huyo mwingine. Utasukumaje ja—jabali huko juu, nusu jengo la mji hewani lililo na uzito wa tani elfu moja. Kile walichokuwa nacho wakati huo kilikuwa ni nguvu za atomiki, kama tu walizo nazo sasa, nao wakajenga. Na hivyo ndivyo walivyoutikisa ulimwengu kutoka kwenye mzingo wake, maana, mbali na

jua, wakautupa kwa upande, kisha wakaleta mvua na—na kuuangamiza ulimwengu kwa maji. Wakati huu watakitupa kiti hicho hicho moja kwa moja kukirudisha kwenye jua na kuutekeza tena; ni kamilifu tu iwezavyo kuwa.

⁹¹ Lakini angalieni katika kuijenga piramidi . . . Sasa, angalieni hili. Una noti ya dola mfukoni mwako? Na—nafikiri nina moja. Kwa hiyo kama ukiangalia nyuma ya noti yako ya dola, ni kwa nini wanayo piramidi inayosema, “Muhuri Mkuu?” Ulipata kuuona kwenye dola yako ya Kimarekani? Um-hum. “Muhuri Mkuu.” Angalieni kwenye piramidi hiyo pia, jinsi ambavyo inaanzia huku chini na inaendelea kupanda juu namna *hii*, uchache, uchache. Basi mliona, jiwe la kufunika hata haliko juu yake. Wala hiyo piramidi haijafunikwa. Kwa nini? Jiwe la Kifuniko lilikataliwa, Yesu Kristo, Kichwa chake, kweli kabisa.

⁹² Sasa, angalieni, katika wakati wa Luther, tuliishia nini? Kuhesabiwa haki, hapa chini kabisa, kuweka mawe ya msingi, Luther; Wesley, tuliamini katika utakaso, kuingia katika uchache; Pentekoste, ingali ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, huku juu katika uchache. Lakini angalieni, Kanisa linaloenda moja kwa moja hata kwenye mwisho wake, moja kwa moja kwenye mwisho wa huo, italibidi Kanisa hilo kuwa kamilifu kabisa kama huduma ya Yesu Kristo, mpaka wakati hilo jiwe litakapokuja, linaingia kikamilifu kwenye huo mfuo. Loo, Haleluya! Loo.

⁹³ Kama mnaweza kulishika na kujua kile ninachozungumzia, huduma yenyewe ambayo Yesu Kristo alikuwa akifanya hapa duniani, itakaporudi, huduma ile ile aliyokuwa nayo, Pentekoste haitalazimika kujipanua yenyewe katika dhehebu, lakini itajichonga yenyewe katika Kristo mpaka lile Jiwe la Kichwa na Kanisa yataingiana. Ndipo yatashikamana sana, hata huwezi kuchukua wembe na kuzunguka upate mwanya mahali yaliposhikamanishwa. Na hivyo ndivyo Kanisa halina budi kuja, kufanana sana na Kristo. Basi angalieni kile kinachotupasa kufanya basi. Kukatilia mbali na kutahirisha na kukatakata, na kufanya na kufinyangwa kuwa katika sura ya Yesu Kristo mpaka Kanisa hilo na hicho Kifuniko viingiane kikamilifu.

⁹⁴ Angalieni mkono wangu kwenye kivuli ukutani. Wakati ukiwa mbali nami, umetawanyika. Unapokuja, unakuwa karibu zaidi. Hakuna vidole vikubwa mno, vinakuwa vidogo zaidi na zaidi na zaidi, vinakuwa vyeusi zaidi na zaidi na zaidi, mpaka kile kivuli, negativu na halisi vinakuwa kimoja. Na hivyo ndivyo ilivyo katika kule Kuja, Kanisa halina budi kujichonga, mpaka halina waa wala kunyanzi ndani yake. Amina. Hiyo hapo Biblia ile ya pili.

⁹⁵ Ya tatu imeandikwa juu ya karatasi kwa sababu huu ndio wakati ule mkuu wa kielimu ambao tunaishi ndani yake. Wala hakuna moja ya hizo itakayohitilafiana na nyingine. Kwa hiyo mnaona, ule mfumo mkuu wa jua unanena juu ya Kristo. Kila

kitu unachokiona kinanena juu ya Kristo kama ukikiangalia tu. Liangalie kanisa siku hizi katika hali yake, dhaifu, limerudi nyuma, limerudi katika ulimwengu. Hiyo inanena juu ya Kristo, jinsi hasa Yeye alivyosema. Angesimama mlangoni na kubisha. Na hilo, aliwekwa nje, wakajiundia dhehebu wakamtupa nje, na kumweka nje; kanuni zetu za imani na kadhalika zilimtupa Yeye nje. Lakini angali anasimama mlangoni na kubisha na kusema, “Kila mmoja nimpendaye, ninamrudi na kumkemea.” Hiyo ni kweli. Kujaribu kuwakatilia mbali na kuwaleta mahali ambapo wakati lile Jiwe kuu la Kufunika litakapokuja, huduma iliyo kanisani na Jiwe la Kifuniko vitashikamana pamoja kabisa kama sumaku. Vitatiwa muhuri moja kwa moja ndani pamoja. Ee, Mungu, tusaide kuwa na... Litakuwako; msijali; litakuwako. Yeye alisema litakuwako. Kwa hiyo hebu na tujandae kukutana na Jiwe lile la Pembeni. Hebu na tupendane na kuyaonyesha maisha yetu ndani ya Kristo na tuwe waaminifu na kudumu pamoja na Neno, hata wakati Yeye atakapokuja tuingiane pamoja kama glovu kwa mkono, namna hiyo, pamoja Naye. Loo, hilo ndilo Kanisa ambalo Mungu anangojea. Naam, bwana.

⁹⁶ Sasa, Yeye alikuwa... Tunatambua kutoka mavumbini sasa, mlango wa 13, hata mlango wa 15, sasa, tunaona. Tulimwacha jana usiku ambapo alikuwa amefanya jambo zuri, Ibrahimu. Ndugu yake Lutu aliyerudi nyuma alishuka Sodoma na akawa mtu mkubwa kule chini na akatoka kwenye mapenzi ya Bwana. Basi inatubidi kutafuta maisha ya raha? Inatupasa kuomba tupate maisha ya starehe? La. Yule mtunzi wa kale alizoea kuandika, aliandika wimbo, “Ni lazima nipelekwe nyumbani Mbinguni kwa maisha ya starehe, huku wengine walipiga vita wapate kushinda tuzo na wakaabiri bahari zilizolowa damu? La, sina budi kupiga vita endapo nitatawala. Zidisha ujasiri wangu, Bwana.” Jambo ndilo hilo.

⁹⁷ Hatuombi tupate jambo rahisi. Siku hizi kanisa linataka tu kwenda kulala na kujipepea kwa namna fulani ya thiolojia ndogo, mwajua. “Naam, tunaamini hilo. Naam, uko sawa; jiunge na kanisa, hivyo tu ndivyo unavyopaswa kufanya. Lete barua yako kutoka kwa Methodisti utuletee sisi Wabaptisti. Na—na—na endapo Waumojia hawatakupokea, sisi Wautatu tutakupokea. Na kwa hiyo, sisi hapa, nautakia heri maskini moyo wako.” Loo, ndugu. Hmm, hmm. Hao si Wakristo. Huo ni uhotara, dini chotara, nilihubiri juu yake sio muda mrefu uliopita.

⁹⁸ Chochote ambacho ni chotara kimechafuliwa. Nayo dini ambayo imefanyiwa uhotara kutoka kwenye Biblia hii ikaingia katika shirika ama dhehebu ama kanuni za imani ya kanisa, ni chotara. Sasa, angalieni, uhotara hutoa sanaa nzuri zaidi, bidhaa ya kupendeza zaidi. Hebu chukua ngano. Tuna mahindi, mahindi chotara, baadhi ya mahindi mazuri sana tuliyoipata

kuwa nayo, bali hayafai kitu. Ukichukua mahindi hayo chotara uyapande tena; hayawezi kujizaa tena.

⁹⁹ Mchapa kazi mzuri sana waliye naye ni nyumbu. Ma—mama yake alikuwa fa—farasi jike, na baba yake alikuwa maskini punda jike, ama maskini punda dume. Nao... nyumbu huyo hawezi kumzaa nyumbu mwingine; hawezi kujizaa tena. Na kile tulicho nacho siku hizi ni kundi la dini ya nyumbu chotara, kweli kabisa, lililozalishwa kutoka kwa kanuni za imani za Methodisti hadi Baptisti na Pentekoste na Presbiteri na madhehebu mpaka hatuna kitu. Kama kuna kitu ninachochukia kukiangalia, ni maskini nyumbu. Ha—hana upendo hata kidogo. Anaketi nyuma, hicho kichwa kikujua kirefu, mwajua, nawe ukizungumza naye, useme, “Tsk. Njoo, jamani, njoo jamani.”

¹⁰⁰ Atasema, “Hoo, hoo, hoo. Siku za miujiza zimepita; tulijifunza hilo katika seminari, hoo. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu, hoo, hoo,” hakuna upendo hata kidogo. Hajui baba yake alikuwa ni nani. Hajui mama yake alikuwa ni nani, wala hawezi kwenda mbele zaidi ya alivyoenda wakati huo.

¹⁰¹ Lakini kitu chochote nipendacho ni chotara wa fa-... farasi mzuri aliyesajiliwa, ukoo mzuri uliosajiliwa, loo, ndugu, ukoo safi. Hivyo ndivyo ninavyoipenda dini, ninapenda dini halisi ya ukoo safi wa Kipentekoste. Wao wanaweza kukwambia mahali walikotoka. Wanajua baba yao na mama yao walikuwa ni nani. Huwaoni na nywele zilizokatwa, na nguo unazomwagiliwa ndani yake, kama namna fulani ya soseji iliyofunikwa na ngozi, ama kitu kama hicho. Sasa, mnavuta sigara, mnaoa wanawake watatu ama wanne, mnatangatanga mkinywa pombe, na kupiga makelele, wakijiita wenyewe Wakristo. Wao hawafanyi hivyo, hiyo ni Pentekoste chotara iliyoingizwa katika dhehebu. Lakini Pentekoste halisi inasimama kwenye mstari wa mbele wa mashambulizi, wanamtetea Mungu, kweli.

¹⁰² Chotara, imekuwa chotara sana katika hii, Marekani imezama sana katika uchotara hata nanii wake... watu wanakuwa machotara. Mnajua hamna budi kurudi kwenye mambo ya asili. Sasa, hebu niwaonyeshe mahali ambapo sayansi inadai ya kwamba tulitoka kwenye uhai wa mnyama; hilo linawavunja-vunja. Kama chochote huzaa... Mwanzo 1:26 ilisema, ninaamini ilisema, “Kila... Kila mbegu na izea kwa jinsi yake.” Kila mbegu kwa jinsi yake nawe ukiichanganyisha mbegu hiyo, haiwezi kujizaa tena. La, bwana, imekwisha wakati... Hiyo inaonyesha ya kwamba kamwe hatukutokana na tumbili na kadhalika, tukizidi kuwa bora zaidi na zaidi. La, bwana, hatukutoka huko. Kwa urahisi tumefanya kwa sura ya Mungu. Sisi ni wana na binti za Mungu.

¹⁰³ Naam, mwanamume na mkewe ni mmoja. Mwanamume, wakati alipofanywa kwa mara ya kwanza, alikuwa ni wote

wawili, katika roho yake, mwanamume na mwanamke pia. Wote wawili walikuwa ni yeye, alikuwa ni mwanamume na mwanamke, peke yake. Lakini wakati Mungu alipomtenganisha kamwe hakwenda... Mwanamke hayuko katika uumbaji wa asili. Yeye ni zaotuka la mwanamume. Yeye aliuchukua mwili kutoka kwenye mwili wa mwanamume na kuchukua sehemu ya kike kutoka kwenye roho yake na kuiweka ndani ya mwanamke, naye ni wa kike, na huyu ni wa kiume.

¹⁰⁴ Unapooona wanawake kama vile katika Marekani leo hii, wakitaka kutenda kama mwanamume, kuna upotovu hapo mahali fulani. Unapomwona mwanamume amekuwa dondoadume sana, anahofia kusimama, “Kamwe sipendi kuwaambia ninyi nyote mahali mnapoelekea.” Wewe ni mhubiri fulani: mwoga, “Sitaki kuwaambia...” Loo, jamani. Mungu anataka wanaume, hiyo ni kweli, anakutaka, kama wewe ni mwanamke, uwe mama wa heshima, iwapo wewe ni mwanamume, uwe mwanamume. Usininii...

¹⁰⁵ Sasa, sikilizeni, ni chotara. Inagandamana, na, jamani, Pwani hii ya Magharibi imejaa huo kila mahali. Mnajua ni kwa nini? Ustaarabu umesafiri kutoka mashariki, magharibi; na kila kitu kilifuatana nao. Wahindi kabla mzungu hajaja pamoja na wanawake wake, pamoja na wiski yake, na pamoja na dhambi yake, waliishi maisha mazuri. Lakini huyu hapa mzungu akaja, mwuaji, mwuaji kinyama, naye akawaua nyati wake na kadhalika, ndipo basi dhambi ikachafua, nayo imekuja na kusimama moja kwa moja dhidi ya Pwani hii ya Magharibi hapa mpaka iko juu zaidi ya anga. Hiyo ni kweli kabisa. Ukienda mbele zaidi, basi utarudi mashariki tena.

¹⁰⁶ Hili ni eneo la makaburi hapa chini kwa ajili ya wahubiri. Hebu mwangalieni Paul Rader na hao wengine wakifia huku chini: Aimee McPherson, hao wote. Ninaye ndugu hapa juu aliyekuwa ni maskini mhubiri mzuri, wakati alipokuja huku, akaanguka. Naye yule kule juu kwenye dini potovu, damu, mafuta na kila namna ya upuuzi ambao hata si wa Kimaandiko. Mungu aturehemu.

¹⁰⁷ Nena kuhusu Sodoma mamboleo, wakati ongezeko asilimia thelathini la upotovu mwaka uliopita, na mambo ya kijinsia. Ninapata barua kutoka kwa akina mama huku pwani juu ya wavulana wao wenyewe wakiwachukua wavulana na wanaenda kuishi pamoja nao vyumbani; wakilia, maskini akina mama kwa ajili ya watoto wao. Mbona ni fedheha. Mtu fulani hana budi kulikemea. Tubuni la sivyo mtaangamia. Kweli. Mrudieni Mungu. Inasikitisha. Mungu aturehemu.

¹⁰⁸ Sasa, si—siwawii radhi walimwengu hao wengine. Ulimwengu mzima uko hivyo. Lakini mnazunguka tu hapa, mkijikwaa kila mahali. Kama nilivyosema, “Tulizoea kwenda huko Paris, bali Hollywood huwauzia mitindo ya—yao sasa.”

Wanawake wetu wamekuwa wabaya sana hata inawabidi kutuma mitindo huko Paris kuwaonyesha baadhi ya vifungua macho. Salaala, jinsi ilivyo, na hiyo imeletwa moja kwa moja katika kanisa letu la Kipentekoste. Mungu aturehemu, ni jambo la aibu. Tubuni la sivyo mtaangamia. Hiyo ni kweli. Ondokeni kwenye mambo ya aina hiyo.

¹⁰⁹ Kujilinganisha na ulimwengu, hivyo ndivyo yule mfalme alivyotaka wakati mmoja. Walitaka—walitaka mfalme katika Israeli maana hao wengine...Maskini yule nabii mwema aliwaendea, kasema, “Ni lini nilipata kuwaambia jambo lolote katika Jina la Bwana, halikutimia? Ni lini nilipata kuchukua pesa zenu? Kama mnataka mfalme mkafanane na hao wengine, mnamkataa Mungu kama Mfalme wenu.”

¹¹⁰ Manapochukua kanuni za imani badala ya Biblia, basi mnalichukua kanisa kwa ajili ya wokovu wenu. Naye Kristo ndiye wokovu wenu. Roho Mtakatifu huliongoza na kulielekeza kanisa. Mungu kamwe hakuwatuma maaskofu na kadhalika kuyaongoza makanisa wala madhehebu. Yeye alimtuma Roho Mtakatifu ku—ku—kuliongoza kanisa. Wazo la Mungu kwake, ninii Yake... Yeye anapaswa kujua, Yeye ni Mungu.

¹¹¹ Sasa, tunamwona pale, baada ya kumfuatilia ndugu yake aliyerudi nyuma na kumrudisha Lutu, ni jambo gani lililotukia, katika mlango wa 14? Mara alipomrudisha Lutu, Lutu alipaswa kujua kutokurudi kwenye kugaagaa huko tena, lakini alirudi moja kwa moja ndani yake tena, “Kama nguruwe aendavyo kwenye kugaagaa kwake, mbwa kwenye matapiko yake,” Biblia inasema. Hiyo ni kweli kabisa. Kama ilimchefua vya kutosha kutapika mara ya kwanza, ingemchefua tena. Mnaona. Loo, kama nguruwe kwenye kugaagaa kwake, na mbwa kwenye matapiko yake, anarudi. Hiyo ni kweli tu kabisa.

¹¹² Pentekoste iliyotolewa huko nyuma miaka arobaini iliyopita, ilifanyiza kanisa la utakatifu, kituo cha nguvu za Mungu, nanyi mnaona jinsi kanuni zenu za imani zilivyowafanyia mara ya kwanza, kisha mnarudi moja kwa moja ndani yake tena. Acheni Roho Mtakatifu achukue mamlaka. Acheni alitawale kanisa. Acheni aingie ndani.

¹¹³ Sio muda mrefu uliopita nilizomewa kwa jambo hilo katika moja ya Kiamshakinywa cha Wafanyabiashara Wakristo, ama, kilikuwa ni chakula cha jioni, mara baada ya...usiku mmoja Ndugu Roberts alikuwa amezungumza, nami nilikuwa ninene baada yake kesho yake usiku. Basi niliponena, nilinena juu ya hilo. Jinsi ambavyo ilikuwa, ya kwamba mambo haya ambayo nimenena juu ya Delila na Samsoni. Na kwa hiyo mmoja wa ndugu zetu aliamka na kusema, “Vema Ndugu Branham, mchungaji wetu alisema wao wanajua hilo, bali hawawezi kusema chochote.” Kasema, “Wakisema, kanisa litawatupa nje mara moja.”

114 Nikasema, “Kuwatupa nje! Afadhali niwahubirie watu watano waliojazwa na Roho Mtakatifu kuliko nchi nzima iliyojaa joto la waliorudi nyuma nusu. Niseme kweli.”

115 Ni kama tu vile msimu wa kuchipusha unavyokuja, maskini mama ndege wenu watatoka hapa nje na kutaga mayai, na kutengeneza kiota, na kuyafunika. Halafu ataninii... Hivyo ndivyo anavyoleta vifaranga wake. Vema sasa, ingawaje iwapo maskini mama huyo wa ndege, huenda akataga kiota kizima cha mayai, na iwapo hajakuwa na mwenziwe hayataanguliwa. Ha—hayana rutuba. Mkondo wa damu hutoka kwenye jinsia ya kiume. Tunajua hilo, ile himoglobini, damu hutoka kwa mwanamume, kwa sababu ilibidi iwe hivyo, maana mwanamke huleta yai. Yeye ni kiangulio bali hana uhusiano wowote na damu ya huyo mtoto. Hiyo ndiyo sababu daima hulichukua jina la baba yake.

116 Hivyo ndivyo Mungu alivyolifanya. Yesu alikuwa... Mtu fulani alisema, “Lakini Yesu alikuwa ni Myahudi.” Yeye hakuwa. “Tumeokolewa na damu ya Kiyahudi.” Sivyo. Hakuwa Myahudi wala Mmataifa; Yeye alikuwa ni Mungu. Mungu alikuwa ndiye Baba Yake. Mungu aliumba Seli hiyo ya Damu pasipo uhusiano wowote na mwanamume yeyote, Myahudi wala Mmataifa. Tunaokolewa na Damu ya Immanueli. “Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya hiyo gharika, hupoteza waa lao lote la hatia.” Hakuna uhotara wowote kulihusu, ni Damu halisi ya kweli isiyoghoshiwa ya uumbaji wa Mungu Mwenyewe, pasipo kujuana kimwili ndani yake.

117 Maskini mama ndege, angeweza kwenda juu ya kiota hiki na kutaga. Anaweza kutaga mayai vema, vivyo hivyo nasi tunaweza kuwa na makanisa; kama tu nilivyosema, “dini yetu chotara.”

118 “Tuna kanisa zuri sana kuliko tulilokuwa nalo. Loo, jamani, linapendeza.” Ninavutiwa na hilo, lakini ndugu, unapowaona wanawake wetu na wanaume katika kusanyiko letu wakienda chini kwenye maskini kule kujipaka rangi na kutenda kwa kawaida, baridi, nao wanawake... Mbona, ilikuwa ni kosa kwa wanawake wa Kipentekoste kujipaka rangi za makucha, ama, kitu hicho wanachoweka usoni mwao kinaitwaje? chochote kilicho, i—ilikuwa ni... rangi ya midomo. Ilikuwa ni kosa kwao kufanya hivyo. Lakini ninaona wanafanya hivyo sasa. Kuna shida gani? Huh?

119 Sikilizeni. Kulikuwa na mwanamke mmoja tu katika Biblia aliyewahi kujipaka rangi usoni mwake, naye huyo alikuwa ni Yezebeli. Mungu alimlisha kwa mbwa kwa kufanya hivyo. Sasa, unapomwona mwanamke aliyejipaka rangi sana, sema, “U hali gani, Binti Nyama ya mbwa?” Hivyo ndivyo ilivyokuwa hasa katika Biblia. Mungu alimlisha kwa mbwa, kwa hiyo Yeye alifanyiza tu chakula cha mbwa kutoka kwake;

Ni kweli kabisa. Tunachohitaji ni uamsho wa Kipentekoste unaoamsha kusafisha kote kote kutoka mimbarani hadi sakafuni mwa kanisa, kusafisha. Tunamhitaji Kristo, ndugu, dada; tunamhitaji.

¹²⁰ Maskini mama ndege ameketi pale na kuyaatamia hayo mayai mpaka anakonda sana hawezi kuruka kutoka kwenye kiota. Hiyo ni kweli. Anaweza kuyageuza kwa uchaji, na, “Loo, jamani, ni yangu,” na kuyafunika, na kuyafunika. Halafu aseme tu, “Vema, ningeenda nikale bali nimekuwa tu, sina budi kuhudhuria shirika la kina mama. Sina budi ku—sina budi kuwa na *hiki* na *kinginecho*.” Mnaona, mpaka akonde sana hawezi kuruka, bali kama...kamwe hayataanguliwa; yamekufa. Yatakaa papo hapo na kuoza.

¹²¹ Hiyo ndiyo shida ya wengi wa wajukuu wetu wa Kipentekoste. Mungu hana wajukuu wowote, kama nilivyowaambia. Mungu hana wajukuu. Yeye anao watoto tu, wana na binti. Lakini sisi Wapentekoste tuliwaingiza watoto wetu, tukawaweka kwenye kitanda cha watoto, nao wakakua, wao ni Wapentekoste tu kwa sababu sisi tulikuwa Wapentekoste; hao ni wajukuu. Mungu hana wowote, wana tu na binti.

¹²² Nalo yai hilo, kama maskini mama ndege huyo, anaweza kuligeuza vyovyote atakavyo, kamwe halitaanguliwa; litakaa papo hapo na kuoza. Na hiyo ndiyo shida tu leo katika makanisa yetu. Sababu ya sisi...wote wamegawanyika katika mashirika na madhehebu mbalimbali. Tuliwaingiza kwa barua, na kuwapa mkono wakaingia, kwa sababu walikuwa ni watoaji wazuri wa pesa kanisani, nao walisaidia kujenga mijengo mikubwa mizuri, na vitu kama hivyo. Wala hawajui zaidi kuhusu Mungu kuliko Mhotentoti anavyojua kuhusu hekaya za Kimisri. Hawataamini katika uponyaji wa Kiungu. Wanamkataa Roho Mtakatifu. Wa—wanakulalamikia kwa sababu unawakemea watu na kujaribu kuwanyosha. Wamekufa, mayai yaliyoza.

¹²³ Jambo zuri kabisa kufanya ni kukisafisha kiota chote na kuanza upya tena. Mfanye mtu awe na uhusiano na Kristo Ambaye yu hai na anapumua. Kweli kabisa. Lisafishe kanisa, kiota, ua vijidudu na kukinyunyizia dawa vizuri sana, na uanze upya tena. Hiyo ni kweli. Mchukue mtu anayelala madhabahuni kule mpaka wamepata ushindi.

¹²⁴ Jana usiku nilifanya wito wa madhabahuni, wenye dhambi watatu ama wanne wakaja madhabahuni, na ilinibidi karibu kuwasihi watu katika kanisa hili lenyewe waje huku na kuomba pamoja na hao watu. Hmm. Halafu ninyi... Msiwapigie makelele Wabaptisti. Ninaweza kushuka Kentucky na kutoa wito wa madhabahuni na maskini mvulana mmoja huko akitafuna kofia yake na chini ya ushawishi, aelekee madhabahuni, kuwe na akina mama wakongwe kumi na watano karibu naye mahali fulani. Akijaribu...Na sasa, hashuki tu

pale chini madhabahuni na kusema, “Na—namchukua Kristo, Mwokozi wangu.” Wanapigana mgongoni mpaka wanapita. Wana kitu fulani wanapotoka huko.

¹²⁵ Tunachohitaji ni kurudi nyuma na kujifunza kile Wabaptisti walicho nacho. Tunahitaji mhubiri mwingine kama Yohana, aliyeweka shoka lake penye shina la mti na kuvunjilia mbali, kutupa . . . kuukata na kuutupa kwenye tanuru. Amina. Naam.

¹²⁶ Akiisha kwenda na kumrudisha ndugu yake, Ibrahimu, akamrejesha ndugu yake, kisha akageuka moja kwa moja akarudi kwenye kitu kile kile tena, mgaagao ule ule. Ndipo baada ya jambo hilo, Mungu alisema, “Ibrahimu. . .”

¹²⁷ Akasema, “Utanifanyia nini, Bwana? Ninaenda. . . Sina mtoto. Sina watoto wowote. Naye mrithi tu wa nyumba yangu ni huyu Eliezeri wa Dameski.”

¹²⁸ Akasema, “Lakini yeye siye mrithi wako. Nilikuahidi ya kwamba utampata mtoto kwa Sara, na hivyo ndivyo itakavyokuwa.” Mungu huliweka Neno Lake; kamwe halitabadilika; halina budi kubaki hivyo. Mungu hufanya hivyo. Na kama sisi ni watoto wa Ibrahimu tunaliamini hivyo. Yale Mungu asemayo, ndivyo hivyo. Hakuna lingine kwake.

¹²⁹ Sasa, yeye alisema, “Nitajuaje, Bwana?” Loo, jambo hili zuri, usi—usi—usilikose sasa. Lisome utakapofika nyumbani: Kuthibitishwa kwa ile—kwa ile karama, kile alichotaka kumpa sasa. Angalia kile alichofanya katika mlango wa 15. Ibrahimu, Yeye alimwita, kasema, “Nenda, ukaniletee nda—ndama mdogo wa miaka mitatu, kisha—kisha uniletee mbu—mbuzi jike wa miaka mitatu, na—na ko—kondoo wa miaka mitatu, kisha uwalette.” Ndipo Ibrahimu akawapasua vipandevipande na kuwaweka chini. Ndipo akasema, “Niletee hua na njiwa mdogo.”

¹³⁰ Lakini hakuninii. . . hivi mliona, hakumkata njiwa wala hua; kamwe hakuwagawanya. Alikata sadaka ya mnyama, alipasua. Lakini hakuwakata hao ndege, hakuwapasua. Mbona? Mungu kamwe habadilishi agano Lake juu ya uponyaji wa Kiungu, kwa sababu huo ulikuwa ni uponyaji wa Kiungu, hua ama—ama njiwa mdogo. Waliking’oa kichwa na kuacha damu itiririke juu ya mwenziwe, ndipo mwenziwe akaachiliwa naye akaruka akipigapiga mabawa yake nayo damu ikirushwa na kulia, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana.” Huko ni kutakaswa kwa ukoma, yale waliyofanya kwa ajili ya utakaso. Mnaona ninii. . . Na huo ndio mfano wenyewe wa Mwenzi wetu, Kristo, akiuawa, Damu Yake juu yetu nasi tunaitawanya kote duniani tukiita, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu.” Mwenzi aliyekufa, Kristo, Ambaye alikufa kwa niaba yetu.

¹³¹ Sasa, kamwe hakuwapasua hao ndege vipande viwili, bali aliwapasua wanyama. Sasa, hii hapa picha nzuri. Siwatakeni

muikose sasa, enyi darasa. Lakini si—sidhani ya kwamba hiyo ingefaa kuraruliwa *hicho*, nitakirarua *hiki*. Vema.

¹³² Sasa, katika nchi ya kale, huko nyuma Mashariki. Sasa, tuna njia mbalimbali ambazo sisi hufanya agano. Sisi Wamarekani hufanya nini? Tunatoka, tuseme, tunaenda kula chakula. Na—nataka kuzungumza, kama, jambo la kibiashara na Bw. Borders hapa, mmoja wa, meneja wa uamsho wetu. Niseme, “Bw. Borders, ningetaka kuzungumzia mambo fulani.” Basi tunafanya nini? Tunatoka tunaenda kula sambusa na kikombe cha kahawa, ama chochote tufanyacho, tunaketi pale na kuzungumza muda kidogo. Ndipo basi tunaenda, tunazungumzia yale tutakayofanya na kusema, “Ungetaka kufanya hivyo?”

¹³³ “Naam.” Nasi tunapeana mikono. Hilo ni agano. Tulifanya aga...tulifanya ahadi mmoja kwa mwingine na kupeana mikono juu yake. Hivyo ndivyo tunavyolifanya. Kama nilikuwa nikimwambia huyu ndugu hapa, “Naja, kukufanyia uamsho, ndugu.”

Naye angesema, “Vema...”

Huenda tumeketi mezani tukizungumza na—kisha tungeamka nami ningesema, “Limekubalika?”

“Limekubalika.” Tupeane mikono sisi kwa sisi. “Uweke hapa.” Ni—ni mapatano; tumekubaliana.

¹³⁴ Sasa, hivi mliwahi kujua jinsi wanavyofanya huko Japani? Wanazungumziana, nao wanachukua chumvi kidogo kutoka kwenye chupa na kurushiana. Hiyo ni—hiyo ni ki—kidumishi, ladha (Mnaona?), chumvi. Wanarushiana chumvi wanapofanya agano mmoja na mwingine.

¹³⁵ Lakini katika wakati wa Ibrahimu wakati walipofanya agano mmoja na mwingine, walilifanya tofauti, sasa, walipofanya agano, mmoja na mwingine, huko—huko Mashariki, katika wakati huo. Sasa, angalia jinsi Ibrahimu...Mungu alithibitisha agano hili papo hapo pamoja naye, basi angalieni vile Yeye alivyofanya. Alimchukua ko—kondoo, ninii...na sadaka, na kuikata vipande viwili, na kuiweka huko nje. Na sasa, angalieni basi, Ibrahimu aliwalinda ndege wasiikaribie, akaiweka hiyo sadaka safi.

¹³⁶ Loo ndugu, wazuie koho wasiikaribie. Hivyo ndivyo ninavyojaribu kufanya sasa. Hmm. Umm! Wazuie maskini koho wa kilimwengu wa Hollywood wasiingie kanisa la Kipentekoste. Hmm. Um-hum. Wazuie...wasiwakaribie wanawake wetu wala ndugu zetu na vitu kama hivyo. Nanyi mnaweza kuwa na ninii zote kubwa, mizaha ya kipumbavu na mambo mnayotaka kusema, acha wawe nayo, huo ndio ufalme wao. Sisi si—sisi si wa ulimwengu huu. Ufalme wetu si ulimwengu huu. Tunaishi hapa kama Wamarekani, bali nafsi yetu inatoka juu. Wakati...Yeye alisema, “Yeye aniaminiye mimi, yuna Uzima wa Milele.” Uzima

huo wa Milele unatoka kwenye neno *Zoe*, nalo *Zoe* ni “Uzima wa Mungu Mwenyewe”. Sisi ni sehemu ya Uzima Wake.

¹³⁷ Hapo mwanzo Yeye alikuwa ni El, Elah, Elohimu, Yule adumuye peke yake. Ndani Yake mlikuwamo na sifa kuwa Baba, kuwa Mwokozi, kuwa Mponyaji. Nayo mambo haya huonyesha tu, kwa ajili ya sifa Zake, mnaona, ndivyo ilivyo. Hilo ndilo linalotufanya. Yeye, kwanza, Yeye aliumba . . . Vema, Yeye hakuwa Mungu kwanza, kwa sababu *mungu* ni “kitu cha kuabudiwa.” Kwa hiyo Yeye aliwaumba Malaika apate kuwa Mungu. Ndipo akamweka mwanadamu kwenye uhuru wa kujichagulia kwa ajili ya utakatifu Wake Mwenyewe, ndipo alipofanya hivyo, basi mwanadamu akaanguka. Ndipo Yeye akawa Mwokozi. Mnaona, inaonyesha tu sifa Zake. Hakuna kitu kilicho nje ya utaratibu, kinaenda, usifikiri ibilisi anamshinda Mungu; Yeye—Yeye ndiye Bosi; Yeye anajua mahali yote yalipo. Hiyo ni kweli. Anajua mahali yalipo.

¹³⁸ “Vema,” unasema, “unafanya nini basi katika kuhubiri?” Yeye alitwambia twende tukatupe jarife ndani na kuwavuta ufukoni. Anajua ni yupi samaki na yupi ni kamba na ni yupi nyoka na kasa na terapini. Anajua yote kuwahusu. Bali walikuwa hivyo tangu mwanzo. Hiyo ni kweli. Ni kazi yetu tu kutupa juya ndani na kuivuta nje, useme, “Hawa hapa, Bwana. Hawa hapa, Bwana.”

¹³⁹ Muda si muda mnajua, maskini Bibi Buibui wa majini anaketi hapo kidogo, anasema, “Ha, siamini hilo. Mchungaji wangu haliamani.” Kisha anajirusha, anajirusha kwa kishindo moja kwa moja kurudi matopeni tena. Hiyo ni kweli.

¹⁴⁰ Ndugu, jamaa huyo wakati alipotoka, kama yeye alikuwa ni samaki kwanza, yeye ni samaki mwishoni mwa safari, naam, bwana. Jina lake liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye alisema, “Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu; mgeni hawatamfuata.” Watalisikia Neno. “Wote niwapendao, ninawakemea na kuwarudi; iweni na bidii, mkatubu, na kurudi.” Huo ndio—huo ndio wakati, huo ndio Ujumbe tunaoupata sasa. “Rudini . . .” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁴¹ Roho zetu zinaingia mle ambako ni kutakatifu na safi. Mioyo yetu inapaswa kuwekwa juu ya . . . shauku zetu juu ya mambo yaliyo juu aliko Mungu. Sisi ni watoto wa Mungu. Sasa, tutaona hapa kwa muda kidogo tu.

¹⁴² Sasa, wakati Ibrahimu alipowazuia wale koho wote wasiikaribie ile—ile sadaka mpaka jua lilipokuchwa; hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya sasa. Kuwafukuza koho wote mpaka—mpaka—mpaka mapambazuko; hivyo tu ndivyo ninavyoweza kusema. Naam, bwana. Sasa, angalieni kile kilichotukia. Na mara alipofanya hivyo, usingizi mzito ukamshika Ibrahimu. Mnaona? Sasa, *usingizi* unamaanisha

“kifo.” Ndipo wakati alipoyafungua macho yake na kuangalia, kulikuwa na tanuru iliyofuka moshi. Hapo ndipo kila mwenye dhambi anapoelekea, ambapo sote tunastahili kwenda. Tanuru inayofuka moshi ikatokea; hiyo ni kuzimu, ambako kila—kila mwanamume na mwanamke aliyezaliwa katika dhambi, akaumbika katika uovu, akaja ulimwenguni akisema uongo, huko ndiko tunakostahili kwenda hasa.

¹⁴³ Lakini angalia, ndipo baada ya hapo, kukaja nuru ndogo nyeupe. Nayo nuru hii ndogo ikapitia katikati ya vipande hivi vya sadaka. Mungu alikuwa akifanya nini? Akifanya agano Lake na Ibrahimu. Loo, ndugu, si kwa matendo sasa, bali kwa neema; hakuna kitu unachoweza kufanya. Yeye anawaonyesha Israeli ya kwamba Yeye—Yeye—Yeye aliwaokoa Israeli kwa neema pasipo matendo. Agano la Ibrahimu halikuwa ati, “Ibrahimu kama utafanya jambo fulani, nitalifanya.” Yeye alisema, “Nimelifanya.”

¹⁴⁴ Mungu anawataka watu waishi kwa neema, sio kwa torati. Tunakuwa wa kisheria sana, hata, “Vema, ingekuwa ni kosa kwangu kuvuta sigara. Ingekuwa ni kosa kwangu kumkosea mke wangu uaminifu.” Ni upendo, ndugu. Sio kwa sababu. . . Kama unampenda Mungu wako, hutafanya maovu yoyote, maana unampenda kupita kiasi. Sio kwa sababu sipaswi kufanya hivyo, sipaswi kufanya hivyo. Ni kwa sababu unampenda sana hutaki kufanya hivyo. “Mwabuduo akiisha kutakaswa hana. . . tena dhamiri, ama, shauku, kufanya dhambi.” Wakati yeye, akiisha kutakaswa katika Damu ya Yesu Kristo, hana shauku tena ya kutenda dhambi; mambo hayo yamemwondokea. Haimbidi kuninii. . .

¹⁴⁵ Baadhi yao husema, “Halidhuru dhamiri yangu.” Mbona, watu wengine hawana dhamiri zaidi ya vile nyoka alivyo na nyonga. Kwa hiyo tunajua ya kwamba—ya kwamba hakuna kitu kama hicho. Si dhamiri kwa vyovote vile; ni roho yako, Roho Mtakatifu wa Mungu. Haya basi. Upendo wako Kwake, unampenda.

¹⁴⁶ Sasa, angalieni, basi, waliandikaje agano zamani za kale? Walichinja sadaka. Sasa, Nuru hiyo ilikuwa ni Mungu. Ilimwonyesha mahali anapopaswa kwenda, baada ya kifo chake anapaswa kwenda kuzimuni, lakini mbele ya hiyo ilienda Nuru hii ndogo nyeupe, ikipitia katikati ya sadaka hizi.

¹⁴⁷ Sasa, katika Agano la Kale, tuseme. . . Njoo hapa Ndugu Borders. Sasa, tutafanya mapatano, mimi na Ndugu Borders, kama vile katika Agano la Kale. Sasa, jambo la kwanza tunalofanya, tunaketi chini hapa nami ninaandika, “Nitafanya jambo fulani, jambo fulani.” Hayo ndiyo mapatano yangu. Halafu tunaichinja sadaka. Tunaipasua, tunasimama katikati ya hiyo sadaka, mimi na wewe. Nasi tunafanya agano mmoja na mwingine, na ndipo tunapofanya hivyo, tunakirarua *hiki*. Sasa,

wakati fulani tutarudi. Nawe uweke sehemu hiyo nami nitaweka hii. Sasa, sisi hapa. Sasa, hicho hakiwezi kulinganishwa. Hakiwezi (Mnaona?), kwa sababu ni karatasi nazo herufi zimekatwa hivi, na matimutimu madogo, na kadhalika. Hakina budi kulingana kikamilifu, hasa.

¹⁴⁸ Yeye alisema, “Kwa jambo hili utajua agano Langu ni nini, Ibrahimu.” Ibrahimu akiwa wa kiroho alijua hilo. Kwa nini? Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya hasa. Yeye alichukua Uzao Wake wa agano, ambapo Uzao halisi ulikuwa ni Yule aliyeahidiwa kwa imani, akatokea kwa Isaka, akatokea Kristo. Kristo alikuwa ni Agano la Mungu. Na yale aliyofanya, Yeye alimchukua akampeleka Kalvari, kama tu Ibrahimu alivyomfanyia mwanawe mwenyewe siku chache baadaye, ama miaka michache baadaye, akiisha kuzaliwa. Yeye alifanya nini? Alimpeleka Kalvari kisha akampasua vipande (Amina.), akampasua. Akaufufua mwili Wake kwenye asubuhi ya Pasaka na kumweka mkono wa kuume wa kiti Chake cha enzi. Lakini Roho aliyekuwa ndani Yake, akatuma chini kwa kanisa. Kwa hiyo kanisa, wakati Agano hili litakapoletwa katika nguvu zake kamili, wakati hilo Agano litakapothibitishwa na Mungu, kanisa, watu wanaoingia kwenye mwili huu hapa wapate kuwa Bibi-arusi Wake, watakuwa hasa Roho yule yule aliyekuwa juu ya Kristo, wakifanya mambo yale yale, huduma ile ile, nguvu zile zile, nalo litakuja pamoja na kuwa Neno kwa Neno vile vile: likilithibitisha lile Agano.

¹⁴⁹ Sasa, angalieni siku hizi; angalieni kile tunachoona siku hizi na mpate kujua. Nilisema nini kuhusu piramidi? Italibidi ichongwe na kuwekwa ndani kikamilifu sana, takataka zote na kila kitu, mpaka jiwe lile la kichwa itabidi kutoshea kikamilifu. Mnaona? Lile jiwe la kichwa lililokataliwa itabidi lirudi.

¹⁵⁰ Lile agano, Uhai uliokuwa katika Kristo uko ndani ya kanisa, Roho Mtakatifu. Yesu alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena; hata hivyo mtaniona, kwa kuwa Mimi. . .” *Mimi* ni “kiwakilishi nafsi.” “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Nazo kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.” Whiu. Hivi hamlioni? Ni kanisa gani la agano lililothibitishwa, ni wale walio na Roho Mtakatifu, hao ndio. . . “Sisi tuliokufa katika Kristo, tunafanyika uzao wa Ibrahimu nasi ni warithi pamoja naye sawasawa na ile ahadi.” Na endapo hujawahi kumpokea Roho Mtakatifu bado, kamwe hujaingia katika agano la Mungu.

¹⁵¹ Mmoja wa ndugu zangu wa Kibaptisti alinijia sio muda mrefu uliopita, juu ya, ndugu fulani aliyeandika kwenye *Sauti ya Uponyaji* kuhusu Malaika wawili walioshuka na manyoya ya sufu, naye akayagusa; wakampeleka kwa Mungu Baba. Na loo. . . Naye akasema, “Vipi kuhusu hili, Billy?”

Nikasema, “Sasa, ngoja kidogo. Kamwe sikuandika makala hiyo. Sina uhusiano wowote nayo.”

Akasema, “Ninaona ya kwamba umeondoka kwenye maskini Maandiko ya kale, ya kimsingi.”

Nikasema, “La, bwana, niko moja kwa moja ndani yake.”

Yeye akasema, “Billy, unataka kuniambia ya kwamba unafikiri hao Wapentekoste wana kitu tofauti na sisi Wabaptisti?”

Nikasema, “La, wana zaidi ya yale mliyo nayo kwa uchache. Unaona?” Nikasema, “Hivyo ndivyo ilivyo; wana mengi zaidi tu yake.”

¹⁵² Hapa sio muda mrefu uliopita nilikuwa huko...Daktari Hegre, huenda ameketi hapa usiku wa leo, mshauri wa Chuo cha Bethany, chuo cha Kilutheri. Yeye aliniandikia barua, na kweli alinikaripia sana: yeye alisema, “Niliendesha maili kumi na tano za dhuruba ya theluji mbaya sana kumsikiliza mtumishi wa Mungu, basi nilipata nini ila mpiga ramli aliye pigwa msasa,” akasema. Na loo, alinirarua tu vipande-vipande, kasema, “Mtu anayewazungumzia watu kama ufanyavyo, na theolojia iliyooza kuliko zote niliyopata kusikia maishani mwangu.”

¹⁵³ Akasema, “Ulisema ya kwamba Shetani haponyi,” kasema, “sasa, tunaye mwanamke kwenye jamii yetu kule, yeye ni—ni—ni mchawi. Amevaa nguo kubwa; anawaelekeza watu watie pesa mle, halafu basi atazichukua na kung’oa baadhi ya nywele zake, na kung’oa mishipa yao, naye ataweka hizo nywele na damu pamoja, na kuteremka kwenye kijito kilicho nyuma yake, anazitupa nyuma yake. Anaanza kuwaendea hao watu, kama akilazimishwa kuangalia kando huo ugonjwa unawarudia hao watu; usiporudi, unaondolewa.” Ndipo akasema, “Tumeangalia, yapata asilimia ishirini ya hao watu wanaponywa. Halafu wewe unasimama mimbarani na kusema ya kwamba Shetani hawezi kuponya.”

¹⁵⁴ Vema, mimi...Wala asingeniita “ndugu.” Alisema, “Nilikuwa nikihubiri kabla hujazaliwa.” Naye, loo, alinikemea kwelikweli. Nikawazia, “Vema, sawa, hiyo ni sawa. Ninathamini hilo.”

¹⁵⁵ Kwa hiyo nikawazia, “Nikiwa na kurasa ishirini na mbili kumjibu kwa angalau ukurasa mmoja nipate kumwonyesha ushirikiano wangu.” Kwa hiyo nikachukua kitabu ki—kidogo, nami nikasema, “Sasa,” nikasema, “Mpendwa Ndugu katika Kristo,” Nikasema, “Salamu za Kikristo kwako.” Kama mtu alihubiri muda mrefu hivyo, anastahili kuheshimiwa, kama amehubiri Injili, hata kama akiwa makosani. Nikasema, “Jambo la kwanza ninalotaka kusema, ninakusamehe yale uliyosema. Sasa, Yesu alisema...

¹⁵⁶ Watu huja kumwona Yeye, na, akatenda mambo yale yale uliyoona yakitendwa, akienda na kuyatambua mawazo ya watu na kuwaambia mambo *yaliyokuwako*, na *yatakayotendeka*, nao wakamwita ‘Beelizebuli, mpiga ramli, ibilisi.’

¹⁵⁷ Naye Yesu akasema, ‘Nitawasamehe hayo, lakini siku moja Roho Mtakatifu yuaja kufanya hivyo nanyi mkisema neno dhidi yake, hamtasamehewa kamwe, kwa hiyo basi, katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.’” Nikasema, “Vipi kama hii ilikuwa ni kweli, basi miaka yako hamsini ya kuhubiri imeenda wapi? Unaona? Ilikufaa nini? Umepotea wala kamwe huwezi kuokolewa.” Nikasema, “Lakini najua ulisema hivyo kwa kutokufahamu.” Mnaona, kwa namna fulani kumfanya kidogo apate kujua ya kwamba sisi hatukuwa gizani.

¹⁵⁸ Kwa hiyo basi, yeye alisema... Nami nikasema, “Lakini wazo lake ni kwamba, yale ninayosoma habari zake, ndugu yangu,” nikasema, “linalonishangaza mimi, ni kwako kusema ya kwamba Shetani anaweza kuponya.” Nikasema, “Yesu Kristo alisema, ‘Iwapo Shetani anaweza kumtoa Shetani, basi ufalme wake umegawanyika juu ya nafsi yake mwenyewe.’ Hiyo ni kweli. Yesu alisema asingeweza kuponya, sasa wewe umesema anaweza, na Yesu alisema asingeweza. Basi ni nani anayesema kweli? Yeye alisema, ‘Neno la kila mtu liwe uongo na Langu kweli.’” Nikasema, “Kwa hiyo, basi, Yesu anasema kweli nami ninalikubali Neno Lake, ndugu yangu.”

¹⁵⁹ Nikasema, “Lakini ingawaje,” nikasema, “hakika, ninaweza kuona mahali huo uponyaji unapokujia.” Nikasema, “Tunao watu nchini siku hizi, wanaoitwa waponyaji wa Kiungu, wanaoenda huku na huku wakisema, ‘Utukufu, ninao uponyaji mkononi mwangu, whiu, mnauhisi?’” La, huuhisi, unauhisi mkono, sio uponyaji.

¹⁶⁰ Yesu kamwe hakusema, “Uliuhisi?” Alisema, “Uliamini?” Hiyo ni kweli. Sio, “Uliuhisi.” Mihemko hii yote na mambo yote, ndugu, ni kitu fulani cha uongo, cha kujibunia. Si Neno la Mungu. “Yeye aaminiye...” Hapo ndipo lilipo. Ni imani katika kazi iliyomalizika. Kristo alikufa, akawaponya pale Kalvari. Akawaokoa pale. Huna budi kulikubali kwa imani kama wengine wetu wanavyofanya. Kweli. Uamini.

¹⁶¹ Haikubidi kuketi pale na kupigapiga na kulia usiku kucha; ungeweza kulia mpaka uingie mvi na kulazwa madhabahuni na kufa. Mpaka utakapoikubali sadaka hiyo ya Damu ambayo Mungu aliitoa kwa ajili yako, umepotea. Sijali jinsi unavyojisikia. Mimi sitegemei jinsi ninavyojisikia; ninajisikia mara nyingi kana kwamba niko nyuma kabisa. Lakini Biblia ilisema nimetimiza matakwa ya Mungu.

¹⁶² Yesu alimshinda ibilisi juu ya Neno. Yeye alisema, “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, yaamuru mawe haya yawe mkate.”

Kasema, “Imeandikwa, ‘Mtu hataishi kwa mkate pekee.’”

¹⁶³ Alimshinda kwa Neno la Mungu, na hivyo ndivyo tunavyomshinda, ni kwa Neno la Mungu, BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli.

Unasema, “Ni mpiga ramli.”

¹⁶⁴ Basi kwa nini Mungu akasema, “Akiwapo mtu miongoni mwenu aliye wa kiroho ama nabii, anaponena na kisha yale asemayo yatimie, msikieni, kwa kuwa niko pamoja naye”? Maandiko haya yote yanakujaje moja kwa moja kufikia siku hii ya mwisho?

¹⁶⁵ Mnaona, kamwe hawafahamu. Mnaona, kamwe hawawezi kufahamu. Ni ufunuo wa Mungu kupitia Neno Lake. Wanakuja... Hawakumwamini Yeye wakati alipokuja. Hawaliamini kanisa siku hizi wakati limekuja katika uwepo wetu. Hawa—hawaliamini kwa sababu haliafikiani na thiolojia yao. Lakini linaaafikiana na Neno. Mungu akilithibitisha Neno Lake kwa ishara zinazofuata, hilo ndilo thibitisho, kama Yeye akisema *hili* nalo linatimia. Kama tukihubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu na mtu fulani aupate, hiyo inathibitisha kwamba ni wa kweli.

¹⁶⁶ Sasa, angalieni, naye Daktari Hegre wakati nilipozungumza naye nilisema... nilipoiandika barua hii, nilisema, “Hakika, nimekuwa Afrika na kuwaona wakiponywa kwa sanamu ya udongo.” Nikasema, “Nimekuwa huko La Salle, Lorraine huko Ufaransa, na kuwaona hao watu wakipanda kwenda kule kwa mwanamke huyo, mwanamke fulani aliyekufa, nikawaona wakiponywa. Kwa nini? Kwa sababu wanaamini wanamkaribia Mungu kupitia kwa sanamu hiyo. Mnaona? Naye Mungu ameweka uponyaji wa Kiungu kwenye msingi wa imani yako.” Hiyo ndiyo sababu Yeye hakuwapasua hua hawa na kadhalika. Mnaona? “Ni juu ya imani yako, kama unaliamini; nao hao watu wanafikiri wanamwendea Mungu. Wamarekani hawa wanafikiri wanamwendea Mungu kupitia mponyaji wa Kiungu. Mwafrika anafikiri anaukaribia kupitia mchawi wake. Huyo mchawi kule juu nyuma ya nyumba yako, hao watu wanafikiri wanamwendea Mungu. Naye Mungu anaitambua imani yao. Hivyo tu.” Lakini nikasema, “Watawajibika kwake, kwenye Siku ya Hukumu, kwa mambo kama hayo.”

¹⁶⁷ Lakini nikasema, “Kilichonishangaza, kama Mshauri wa Kilutheri, kuweka msingi thiolojia yake juu ya ujuzi badala ya Neno la Mungu.” Uh-huh, nilifikiria nitamwacha ajue hatukuwa wa bandia kwa vyovyote vile. Mnaona? Angewezaje kuweka msingi ujuzi wake juu ya Ne-... Angewezaje kuweka msingi mafundisho yake juu ya ujuzi fulani, mwanamke fulani aliyefanya jambo moja ama lingine, badala ya yale Mungu aliyosema? Mungu alisema Shetani hawezi kuponya, na hilo latosha kwangu. Hiyo ni kweli.

¹⁶⁸ Mnajua nini? Yeye alinialika. Akasema, “Ndugu Branham...” Sasa, tulitoka tukaenda huko nje, nasi tulikuwa na idadi kubwa karibu kama iliyo hapa, kwa ajili ya chakula cha kutwa, kundi lote la wanafunzi lilikuwa ndani. Yeye akasema, “Sasa, Ndugu Branham,” akasema, “na—na—nataka kukuuliza jambo fulani.” Kasema, “Sikumaanisha yale niliyosema,” lakini kasema, “sisi tuna njaa na kiu hapa cha Mungu.”

Nikasema, “Hilo ni jambo zuri; hilo ni sawa, Daktari.”

¹⁶⁹ Naye akasema, “Hili hapa ndilo tunalotaka.” Na kama ninyi nyote mkitaka kumwandikia juu yake, andika tu Daktari Hegre kwenye—kwenye...ninajaribu kukumbuka huko... Minneapolis, Minnesota, Chuo cha Bethany. Na kwa hiyo yeye...Na muandike tu na kumwuliza. Naye alisema, “Vema, tunamwonea Mungu kiu hapa,” kasema, “tunamtaka Mungu.” Kisha akasema, “Tunasoma kuhusu Wapentekote,” ndipo akasema, “wasemaje juu yao? Sasa, wewe ulikuwa ni Mbaptisti.”

¹⁷⁰ Nikasema, “Naam, bwana, nilikuwa.” Nikasema, “Mimi ni Mbaptisti wa Kipentekote sasa.” Naye akasema...Nikasema, “Mimi ni Mbaptisti aliye na tukio la Kipentekoste. Mnaona,” nikasema, “Pentekoste, Daktari, si dhehebu. Huwezi kuiundia Pentekoste dhehebu; ni tukio (Mnaona?) kwa Mmethodisti, Mbaptisti, Mkatoliki, na kila mtu; ni tukio. Sio tu kufikia kwenye...Waassemblies sio tu walio na Roho Mtakatifu. Waumoja sio tu walio na Roho Mtakatifu, Foursquare. Ni yeyote atakaye, na aje. Jambo ndilo hilo.” Yeye alipendezwa na hilo. Nami nikasema, “Hivyo ndivyo ilivyo.”

¹⁷¹ Naye akasema, “Vema, ninataka kukuuliza jambo fulani.” Kasema, “Nimewaona wakipiga viti mateke, na kupiga taa za dirishani, na kuanguka sakafuni.”

Nikasema, “Naam, bwana.”

Kasema, “Ni kitu gani hicho?”

Nikasema, “Roho Mtakatifu.”

Yeye akasema, “Ati Roho Mtakatifu?”

¹⁷² Nikasema, “Naam, wanapulizia mvuke wao wote nje kutoka kwenye filimbi badala ya kuukusanya pamoja upate kulifanya gurudumu libingirike. Mnaona, naam, kweli hawajui jinsi ya kuninii...Mnaona, kama kamwe ungaliwafanya kusimama mahali fulani na kuweka baadhi ya hizo—baadhi ya nguvu hizo kwenye...mvuke katika valvu kuufanya usukume mkokoteni na kuwa na ishara, maajabu, miujiza, na moto mkuu juu ya nafsi namna hiyo, wakisonga mbele, ungefanya kitu fulani.” Mnaona? Nikasema, “Lakini wanautoa wote kutoka kwenye filimbi, na ni hayo tu.” Nikasema, “Ni vizuri kutosha wana ninii...na kuonyesha kwamba wanao mvuke kwa vyovyote vile.”

Na kwa hiyo yeye alisema, “Vema, unafikiri sisi Walutheri tuna nini?”

¹⁷³ Nikawazia, “Loo, loo. Ee Bwana, U—Unisaidie hapa.” Ndipo Bwana akanipa kitu fulani. Hakika wana yapata ekari elfu kadhaa kule za mahindi na kadhalika ambayo wana—wanayakuza. Hilo kundi la wanafunzi, endapo hawawezi kulipia karo shuleni, basi wanaweza kufanya kazi mashambani. Kwa hiyo wao—wao walikuwa na zao hili la mahindi makubwa huko nje. Ndipo nikasema, “Daktari Hegre, asubuhi moja kulikuwako na mtu aliyekuwa amelima shamba lake naye alikuwa na shamba kubwa zuri la mahindi. Basi akapanda mahindi mle na kila asubuhi yeye angeenda na kuyaangalia hayo mahindi. Hatimaye asubuhi moja akaenda, naye akaona majani mawili madogo.” Mtu yeyote aliyewahi kupanda mahindi, hivyo ndivyo yanavyochipuka. “Ndipo mtu huyo akasema, ‘Mungu asifiwe kwa ajili ya zao langu la mahindi.’” Nikasema, “Sasa, kwani yeye alikuwa na zao la mahindi?”

Akasema, “La.”

¹⁷⁴ Nikasema, “Lakini kwa uwezekano alikuwa nalo. Mnaona? Kwa uwezekano alikuwa nalo.” Nikasema, “Hiyo ilikuwa ni ninyi Walutheri kwenye marekebisho ya kwanza.” Nikasema, “Hatimaye hayo yaliendelea kukua zaidi na zaidi, hata kishada kikatokea juu yake. Na hicho kilikuwa ni Wamethodisti. Ndipo Wamethodisti wakaangalia chini kwenu Walutheri, kasema, ‘Nyinyi nyote hamna kitu chochote. Sisi tunaamini katika utakaso; ninyi nyote mnaamini tu katika kuhesabiwa haki. Mnaona, hata hamko ndani yake.’

¹⁷⁵ “Lakini ngoja, muda si muda mwajua, kishada hi—hi—hicho ni chavua, ilibidi kitumie lile jani tena. Kwa hiyo chavua ilianguka ikaingia kwenye—kwenye jani, nalo likazaa kanisa la Kipentekoste.” Nikasema, “Ni—ni punje ya asili, kama ile iliyoingia ardhini. Punje ikatokea.” Nikasema, “Tuna kuvu nyingi kwenye suke, lakini hata hivyo kuna punje mle pia.” Nikasema, “Hiyo—hiyo ni kweli.” Nikasema, “Wao... tuna kuvu nyingi sana juu yake; nitakubali hilo.” Lakini nikasema, “Ilikuwa ni punje ya asili iliyoingia ndani.”

¹⁷⁶ Nami nikasema, “Basi unajua vile lile suke lilivyosema? Kasema, ‘ewe maskini Mlutheri, nawe maskini Mmethodisti, hamko ndani yake hata kidogo.’” Lakini nikasema, “Hata hivyo, uhai ule ule uliokuwamo katika yale majani ndio uliofanyiza kishada, halafu majani na kishada yakafanyiza suke.” Nikasema, “Kitu pekee lilicho kanisa la Kipentekoste, ni kanisa la Kilutheri lililoendelea (Amina.): uhai ule ule, bali mwingi zaidi.”

¹⁷⁷ Hiyo ndiyo shida iliyopo usiku wa leo, ndugu. Usijaribu kurudi chini mizizini tena, kuwa uhai, endelea; panda juu zaidi. Hivyo ndivyo nilivyomwambia ndugu yangu Mbaptisti.

Yeye alisema—alisema, “Ndugu Branham, Ibrahimu alimwamini Bwana na ikahesabiwa kwamba ana haki.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli kabisa.”

¹⁷⁸ Akasema, “Ndugu Branham, ninataka kukuuliza swali moja.” Jamaa huyu alikuwa ni daktari, nami, bandia. Kwa hiyo akasema, “Ninataka kukuuliza swali moja.” Akasema, “Mtu angeweza kufanya nini ila kuamini; hivyo tu ndivyo angaliweza kufanya.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.”

Akasema, “Basi kama tunamwamini Mungu, tumempokea Roho Mtakatifu tunapoamini.”

¹⁷⁹ Nikasema, “La, hilo halitaafikiana na mafundisho ya Paulo.” Nikasema, “Paulo alisema katika Wagalatia 1:8, ‘Kama Malaika alifundisha kitu kingime chochote na alaaniwe.’ Paulo aliwaambia, Matendo 19, yeye alisema, ‘Mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?’ Sio *wakati* mlipoamini, bali *tangu* mlipoamini. Tulisema ya kwamba, ‘Hatujui kama kunaye Roho Mtakatifu yeyote.’ Akasema, ‘Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani?’ Kasema, ‘Wa Yohana.’ Kasema, ‘Yeye alibatiza tu kwa toba, akisema tunapaswa kumwamini Yeye atakayekuwa, sio kwa ondoleo la dhambi.’ Basi waliposikia haya walibatizwa katika Jina la Yesu Kristo, naye Paulo akaweka mikono yake juu yao, ndipo Roho Mtakatifu akawashukia, nao wakanena kwa lugha na kutabiri.”

“Vema,” akasema, “vipi kuhusu hilo?”

¹⁸⁰ Nikasema, “Angalieni, kama mkisema mnayo imani katika Mungu wala Yeye kamwe... Mnaona, Ibrahimu alimwamini Mungu ndipo Mungu akampa tohara kama ishara, ama thibitisho, ya kwamba Yeye alikuwa ameikubali imani yake,” nami nikasema, “Endapo Yeye hajakupatia ubatizo wa Roho Mtakatifu bado, kamwe hajakupa thibitisho (Amina.), kwamba wewe ni uzao wa Ibrahimu.”

¹⁸¹ Nasi tunatiwaje muhuri katika Ufalme wa Mungu? Waefeso 4:30 inasema, “Msimhuzumishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwaye mmetiwa muhuri hata Siku ya ukombozi wenu.” Amina. Madaraja yote yameteketezwa nyuma yako. “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri (Wewe ni uzao wa Ibrahimu.), mpaka Siku ya ukombozi wenu.” Loo, jinsi ninavyopenda hilo, Mungu akitoa thibitisho la ishara ya kwamba alikuwa ameipokea imani yake.

¹⁸² Naye angesema nini kuhusu jinsi Yeye angeiendeleza imani hii ya ule mzao? Yeye alimpasua Kristo vipande, akaupeleka mwili Wake juu na kuuweka kule kama sadaka iliyolowa Damu, ameketi mkono wa kuume wa Mungu, akifanya uombezi juu ya maungamo yetu: Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, yeye yule jana, leo, na hata milele. Nayo Roho Wake aliyekuwa juu Yake amerudi kanisani akifanya kazi zile zile alizofanya Yeye, akiendeleza jambo lile lile, akilichonga

kanisa kwa ajili ya lile Jiwe la Kichwa lipate kuja juu yake siku moja. Haleluya!

¹⁸³ Loo, ninajisikia kubarikiwa. Mtaniita “mtakatifu anayejibingirisha” kwa vyovyote vile, kwa hiyo afadhali muanze. Hii hapa huko juu. Ninapomwona huyo Mtu mmoja mkamilifu ameketi kule, Gavana, na Mtawala, na Mungu juu ya wote, Juu ya jengo, ameketi huko ng’ambo kwenye ile piramidi, zile ninii kuu...nguvu kuu, Mungu mkuu, akishuka kutoka Mbinguni, ameketi, akijishusha chini Mwenyewe miongoni mwa mawe haya, yaliyowekwa pale. Na wakati Luther alipokuwa tu na kiasi fulani cha imani, Wesley alikuwa tu na kiasi fulani, Pentekoste ilikuwa tu na kiasi falani, lakini Yeye anayafunganisha hayo mawe pamoja ambapo yanaingiana jiwe kwa jiwe. Haleluya! ninaliona likitendeka: Mungu akithibitisha kwa Roho Mtakatifu wa Mungu akitenda kazi kanisani na akifanya kazi zile zile na maisha aliyoishi Yesu.

¹⁸⁴ Ikiwa ni mpichi, utazaa mapichi. Iwapo ni mtofaa, utazaa matofaa. Sijali jinsi upande wa nje unavyoonekana; inaonyesha uhai ulio ndani, ndio unaozaa tunda lake. Ukichukua mzabibu, uweke uhai wa mboga ndani yake, utazaa maboga. Kisha ukiubadilisha mara moja na kuchukua mboga na kuweka uhai wa mzabibu ndani yake, utazaa zabibu. Uhai wowote ulioko ndani yake, sijali una jina gani, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste, na wowote ule. Hebu chukua uhai wa mboga na kuuweka ndani ya mzabibu, utazaa maboga. Kama hili ni kanisa la Kipentekoste, mna uhai wa kale wa mboga ndani yake, uondoeni na mpate kurejeshwa kwa chanjo. Amina. Ninaona mna miti hapa juu inayozaa karibu matunda tisa mbalimbali ya aina ya chungwa. Niliiona huko Arizona hivi majuzi; kulikuwako na mchungwa uliokuwa na malimau na kila namna ya matunda aina ya chungwa, mbalungi. Hivyo ndivyo ilivyo.

¹⁸⁵ Yesu alisema, “Mimi ndimi Mzabibu, nanyi ni matawi.” Hiyo ni kweli. Na kama tawi la kwanza... Sasa, kumbukeni, mzabibu hauzai tunda; tawi ndilo linalozaa tunda. Sasa, kama tawi hilo la kwanza lilitokea na kuzaa kanisa la Kipentekoste, wakaandika Kitabu cha Matendo nyuma yake, kama tawi hilo likipata kuzaa lingine, litakuwa ni aina ile ile ya kanisa la Kipentekoste, litakuwa na ishara zile zile na maajabu yale yale.

Sasa, lakini mnasema, “Vipi kuhusu haya mengine?”

Yamepandikizwa.

“Vipi kuhusu Wamethodisti? Vipi kuhusu Wabaptisti? Vipi kuhusu wanaojiita Pentekoste?”

¹⁸⁶ Miti iliopandikizwa. Haizai lile tunda. Mbona, hawaninii... Wanajipeleka hapa nje na kujitamalaki, “Sisi ni *fulani na fulani*; hatutakuwa na uhusiano wowote nanyi.” Hayo si maisha ya Kristo. Yeye alikufa apate kuwaokoa adui Zake, alinyosha

mikono, hata akawaombea; mate yakining'inia usoni Mwake, na kuwaombea wapate kuokolewa. Loo, naam. Mnaona?

¹⁸⁷ Lakini ni kitu gani? Ni kitu gani kinachofanya hivyo...? Kitu gani? Hivi hicho...? Ni tunda la aina gani lile limau lililopandikizwa linalozaa kwenye mchungwa huo? Halizai machungwa; linazaa malimau. Na hivyo ndivyo kanisa linavyofanya. Linazaa Wamethodisti; linazaa Wabaptisti; linazaa Mpresbiteri. Lakini kama mzabibu huo, wenyewe, ukizaa tawi, linazaa machungwa. Ni la asili likitoka kwenye... Lakini hayo makanisa yanastawi na kuishi na kupata kibali na uhai kupitia Kristo ambao umepandikizwa mle. Lakini huo mti halisi wenyewe ni Roho Mtakatifu anayemzaa mwanamume aliyezaliwa mara ya pili, mwanamke aliyezaliwa mara ya pili, nguvu za kufufuka zikiishi ndani yao. Mnaona? Amina.

¹⁸⁸ Yeye alithibitisha hilo, akamwonyesha yale Yeye angefanya, jinsi ambavyo Yeye angemrarua Mwana Wake Mwenyewe; akamwachilia mwanawe hapa katika Mwanzo—Mwanzo 22:14. Tunaona ya kwamba alimwachilia mwanawe pale, akimwonyesha yale Yeye angefanya. Msalaba Wake mgongoni Mwake, tutalifikia kesho usiku, wakati akipanda kwenda Kalvari; msilikose.

¹⁸⁹ Sasa, angalieni, sasa tutapata tamshi moja zaidi hapa. Ninaona nina kama dakika tatu. Sasa, katika mlango wa 17, hebu tupate hili; hili ni zuri. Angalieni. Mara tatu Yeye alitaja juu ya kuthibitishwa kwa lile agano. Mwanzo 13:14, wakati alipojitenga, akatii, ndipo Yeye akamwambia, nitakufanya kama mchanga wa—wa pwani. Halafu Mwanzo 15 hapa, kama nyota za mbinguni. Mwanzo 17:1, Yeye alimtokea baada ya jaribio kuu, ambapo Sara alikuwa ameruka mstari. Mungu angalimwua Sara. Loo, hili hapa jambo la kupendeza. Wakati yeye alipotilia shaka...

¹⁹⁰ Wakati Sara alipomtilia Mungu shaka, Mungu angalimwondosha, bali asingeweza kufanya hivyo. Kwa nini? Yeye ni sehemu ya Ibrahimu. Hiyo ndiyo sababu tunapofanya kosa, Mungu angetuua. Nisingeweza kuja hapa na kuhubiri uamsho, hakuna mhubiri mwingine angaliweza; kamwe msingeweza kuwa na uamsho. Mngekatiliwa mbali milele, bali Yeye hawezi kufanya hivyo. Yeye anamkata Mwana Wake Mwenyewe kama akifanya hivyo. Mnaona? Kwa kuwa mke ni sehemu ya mumewe; si wawili tena; ni mmoja. Kwa hiyo asingalimdhuru Sara pasipo kumdhuru Ibrahimu. Kwa hiyo ilimbidi kumwingiza Sara ndani. Hivyo ndivyo Mungu anavyotufanyia. Dhambi zetu, angalituacha zamani sana, lakini tuko ndani ya Kristo. Amina. Mnaona, kwa hiyo Yeye—Yeye hutusamehe dhambi zetu. Sara, makosa yake yote...

¹⁹¹ Basi baada ya Ibrahimu kupitia kwenye jaribio hilo kubwa naye alikuwa na mwanawe, Ishmaeli, ambaye alikuwa...

kabisa, Mungu alimwambia amsikilize Sara. Lakini alimzaa mwana huyu, baada ya jaribio hilo kuu. Ndipo akakutana naye na—na mlango wa 17 wa Mwanzo, liandikeni mkalisome mtakapofika nyumbani, sina wakati wa kuligusia ila dakika moja tu. Yeye alimtokea katika Jina la Mwenyezi Mungu. “Mwenyezi” linatokana na neno la Kiebrania la *El Shadai*. Shadai, *Shad* linamaanisha “titi la mwanamke.” Shadai ni wingi, mbili. Ndipo akamtokea, “Mimi ni Mungu mwenye matiti.”

¹⁹² Loo, ni faraja jinsi gani kwa mzee. “Nitampataje mtoto huyu, Bwana? Mimi nina umri wa miaka mia moja.” Alikuwa na tisini na tisa. Kwa hiyo yeye akasema, “Vipi mimi, mtu mkongwe, na mwanamke wangu hapa—hapa ambaye Wewe uliniambia nitamzaa huyo mtoto kwake, yeye ana tisini nami, ama, themanini na tisa, angekuwa, nami nina tisini na tisa. Inawezaje. . .”

¹⁹³ “Lakini mimi ni Mwenye matiti,” Agano Jipya na la Kale pia. “Nilijeruhiwa kwa makosa yenu; kwa kupigwa Kwangu mliponywa.” Loo, Mwenye matiti. Titi ni la nini? Kwa ajili ya mtoto anayesumbuka. Hebu mchukue mtoto mchanga ambaye ni mgonjwa na anahangaika, mama anamchukua, anamweka kifuani mwake. Yeye hunyonya nguvu za mamaye, ananyonya hata anarudisha afya yake.

¹⁹⁴ Sasa, kama sisi sote tumelemazwa na dhambi na kuingia kwenye mitindo ya Hollywood, mbona tusije tu kwa El Shadai? Ni wangapi wangetaka kuona kanisa halisi lililojazwa na Roho Mtakatifu hapa, nguvu tu za Mungu? Hakika. Vema, tunafanya nini? Vema, Yeye ni El Shadai, Mwenye matiti; ukitaka wokovu, egemea titini Mwake ukanyonye nguvu zako za kiroho kutoka kwa Neno Lake. Hili hapa Titi Lake, Agano Jipya na la Kale pia. Keti chini, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Maziwa yale yale yanayotoka kwenye titi la mama mmoja hutoka kwa huyo mwingine, kweli kabisa; ila tu ni hatua zake mbili mbalimbali. “Alijeruhiwa. . .” Ikiwa wewe ni mgonjwa, mbona usishikilie tu kwenye titi Lake la ahadi. “Nilijeruhiwa kwa makosa yako; kwa kupigwa Kwangu wewe uliponywa.” Unahitaji nini usiku wa leo? egemea tu kwenye titi Lake.

¹⁹⁵ Na jambo lingine, uliona? Yeye. . . ile *El* linamaanisha “mwenye nguvu”; *Shadai*, “Yule a—ajitoshelezaye, Mpaji Uzima, Mwenyezi, Mwenye nguvu.”

“Ibrahimu, wewe una umri wa miaka mia moja, mkongwe na dhaifu; bali mimi ndimi Nguvu zako.” Hiyo. . .

¹⁹⁶ Mtoto mdogo wakati anaponyonya, si kwamba tu. . . Lakini ni mshibishaji. Mnaona? Mtoto mchanga kwenye titi la mamaye hushiba. Anaweza kuwa analia, maskini tumbo lake linauma, na kurusha mateke, na maskini nguvu zake zimekwisha, bali atakaa pale pale kwenye maskini titi la mamaye namna hiyo na kuacha

kulia, kuvuta kamasi, kuvuta kamasi, ananyonya, anaendelea, atakuwa mzima. Kwa nini? Kwa sababu ameshiba.

¹⁹⁷ Na wakati ninapoweza kuwaonyesha katika Biblia hii ya kwamba Yeye husamehe maovu yetu yote (Ee Mungu), huyaponya magonjwa yetu yote, hebu niishikilie tu hiyo ahadi na kusema, “Baba Mungu, mimi ni mnyonge; ninakuhitaji Wewe. Ninajua ya kwamba Wewe hulitimiza Neno Lako. Wewe ni El Shadai. Ninakuamini Wewe, Bwana. Nijaze na Roho Wako. Nioshe katika Damu Yako. Nirejeshe, Ee Bwana, na unijaribu. Jalia niegemee kifuani. Mimi ni mtoto Wako; nilizaliwa Kwako lakini nikawa dhaifu, bali Wewe ndiwe Mpaji nguvu wangu. Uliahidi ya kwamba ungefanya jambo hilo, nami nitashikilia tu papa hapa, Bwana, nami nitaridhika ya kwamba Wewe utanijaza na Roho Wako, unisafishe katika Damu Yako, uniondolee hukumu yangu yote, uponye mwili wangu na kunipa afya.”

¹⁹⁸ Ni ahadi jinsi gani kuthibitisha ahadi Yake kwa Ibrahimu, “Mimi ni El Shadai.”

¹⁹⁹ “Vema Ndugu Branham, mimi—mimi ni—mimi ni kahaba. Mimi ni—mimi ni mlevi. Mimi ni—mimi ni mlevi sugu. Mimi ni hawa weng-...”

²⁰⁰ Sijali kile ulicho. Njoo moja kwa moja kwa El Shadai. Kama nguvu zako na matumaini yote yamekwisha, Shirika la Kushughulikia Walevi limekukatia tamaa, daktari amekukatia tamaa, hakuna kitu kinachoweza kufanywa kwa ajili yako, Yeye ni El Shadai, Mwenye nguvu. Egemea kifuani mwake na unyonye upate kushiba. Yeye atalitimiza. Hivi hutampenda?

Nampenda, (Kwa nini nisimpende?) Nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa wakati tukiimba kwa utulivu.

Na... (Kwa utulivu na uchaji kweli)
Nampenda (Sasa, hebu Roho Mtakatifu aseme nawe.)

Kwani (Jambo ndilo hilo.) Yeye... (Unajua Yeye alikualika? Kama unahangaika, hujui mahali unaposimama, unasema, “Mimi ni mfuasi wa kanisa.”)

Na kunu-... (Hujui uwe ni wa dhehebu gani; mbona usije tu kwa El Shadai sasa?
“Nimemtafuta Roho Mtakatifu muda mrefu, Ndugu Branham, lakini usiku wa leo naja.”)

Kwenye...

²⁰¹ Mwaweza kuinua mikono yenu na kusema, “Niombee Ndugu Branham, naja.” Mungu akubariki, mwanangu. Mungu

akubariki, dada. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, ndugu.

Na . . . penda, nampenda,
Kwan- . . .

Sasa, hii si hadithi ya uongo, hii ni kweli; Roho Mtakatifu yupo hapa.

. . . pe- . . .

Wewe ni mwenye dhambi na ungetaka Mungu kukuokoa usiku wa leo? Inua mkono wako, useme, “Niombee.”

Na kununua . . . (Mungu akubariki, ndugu.)
wok . . . (Usingeweza kuinua mkono wako
isipokuwa Yeye . . . “Hakuna mtu awezaye
kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu.”)
Mtini Kalvari.

²⁰² Hebu tuuvumishe. Sasa, wakati mnapouvumisha, ninawataka mgeuke, mpeane mikono na mtu fulani karibu nawe na kusema, “Niombee, ndugu,” ama, “dada,” yeyote utakayempa mikono, mtu fulani anayeketi karibu nawe, useme, “Niombee.”

Kwa utulivu sana sasa.

Kwani Yeye . . . (Jambo ndilo hilo, kwa utamu,
ninyi Wamethodisti, Wabaptisti, ninyi nyote
pamoja. “Niombee, ndugu, niombee.”)
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²⁰³ [Ndugu Branham anaanza kuvumisha—Mh.] Sasa ombeni. Ulisema utamwombea jamaa huyo mwingine, sasa mwombee. “Bwana, jalia nikutane na mwanamume huyo niliyempa mikono, ama mwanamke huyo, jalia nikutane nao Utukufuni, Bwana. Kama nafsi zao haziko sawa, zifanye sawa, Bwana. Huyu mwanamume ameketi hapa karibu nami usiku wa leo; huyu mwanamke ameketi hapa. Huyu mwanamke ananiombea, ama huyu mwanamume ananiombea. Nisaidie, Bwana, nisaidie.”

Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²⁰⁴ Sasa, wakati mkiomba, mkiwomba Mungu; kama wewe ni mgonjwa, mbona usiweke mkono wako juu ya mtu fulani anayeketi karibu nawe na kumwombea. Waache . . . Hivi wewe . . . Sasa, wewe waombee; watakuwa wakikuombea. Wekeaneni mikono sasa. Sasa, umekiri ya kwamba ulimtaka Roho Mtakatifu, ulitaka wokovu. Sasa, kama mnataka uponyaji, wekeaneni mikono. Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

²⁰⁵ Mbona msiwekeane mikono iwapo wewe ni mwaminio, ukisema, “Bwana, mponye mwanamke huyu anayeketi karibu

nami? Mponye mwanamume huyu. Wananiombea, Bwana. Ninawataka waniombee, kwa hiyo ninaweka mikono yangu juu yao.” Mungu huyajibu maombi yenu. Jambo ndilo hilo. “Ombeaneni mmoja kwa mwenzake. Mkiungama makosa yenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana mmoja kwa mwenzake, mpate kuponywa. Kwa kuwa maombi ya bidii ya mwenye haki yana nguvu tena yafaa sana.” Waponye, Bwana.

²⁰⁶ Mchungaji, njoo hapa umalizie maombi haya. Mnapoombeana, endeleeni tu kuomba, Nitamwomba mchungaji atuongoze katika maombi. Mungu awabariki.



AGANO LA IBRAHIMU KUTHIBITISHWA SWA61-0210

(Abraham's Covenant Confirmed)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Ijumaa jioni, tarehe 10 Februari, 1961, kwenye First Assembly Of God Ya Long Beach huko Long Beach, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org